

# Sauti ya Siti



TOLEO LA. 39

ISSN 0856 - 230 X

SEPTEMBER 2016

## Unywaji Pombe unaathiri familia



# YALIYOMO



'Mume mlevi alinifanya nilache nyumba yangu'



Baa zinasababisha maadili kuporomoka



Wakati mwingine, ugomvi ndani ya familia husababishwa na pombe

- Pg 4 'Mume mlevi alinifanya niache nyumba yangu'
- Pg 7 Ukweli halisi kuhusu vilabu vya usiku
- Pg 9 Baa zinasababisha maadili kuporomoka
- Pg 12 Utitiri wa baa jijini: Je serikali inapata kodi stahiki?
- Pg 13 Changamoto zinazowakumba wahudumu wa baa Dar
- Pg 16 Sera ya Vileo inahitajika kuthibiti unywaji holela
- Pg 18 Ulevi unachangia ajali za barabarani
- Pg 20 Ulevi wakatisha ndoto za vijana
- Pg 22 Mikumbo inavyowavuta vijana kwenye ulevi
- Pg 24 Pombe inaleta migogoro ndani ya familia

TAMWA



BODI YA  
UHARIRI

**Sauti ya Siti**

Mkurugenzi Mtendaji - TAMWA  
Edda Sanga

Mhariri  
Deogratias Mushi

Usanifu  
Gurnam Ajit

Chama cha Wanahabari Wanawake  
Tz  
S. L. P 8981, Sinza - Mori, Dar es Salaam  
Simu: +255 22 2772681  
Nukushi: +255 22 2772681  
Barua Pepe: tamwa@tamwa.org  
Tovuti: www.tamwa.org

Ofisi za Zanzibar:  
S. L. P 741, Mombasa, Zanzibar  
Simu: +255 24 2232263  
B.Pepe: tamwazanzibar@tamwa.org

# TAHARIRI

## Taifa linahitaji Sera ya Vileo haraka

**K**wa bahati mbaya sana, matumizi ya vileo katika jamii ya Kitanzania yameanza kuwa sehemu muhimu ya maisha ya watu, kwa sababu maeneo ya kuuza pombe yanazidi kuongezeka sehemu tofauti nchi nzima.

Kwa mfano, maeneo yote mijini na vijijini kuna kiasi kikubwa cha utengenezwaji wa pombe na unywaji wake miongoni mwa watu wa kada tofauti, pasipo kujali umri na jinsia.

Inakadiriwa kwamba zaidi ya asilimia 90 ya vileo vinavyotumiwa na watanzania vimetengenezwa majumbani au katika sekta zisizo rasmi.

Kwa upande wa Tanzania Bara kwa mfano, pombe huuzwa kwenye baa, hoteli, migahawa, na maduka makuu pasipo mazuio ya aina yoyote ile.

Zanzibar ni tofauti, na ilivyo ni kwamba, tofauti na hoteli kubwa zinazouza vileo, kwa ujumla migahawa midogo inayomilikiwa na Waislamu pombe haiuzwi.

Tabia za unywaji zimewafanya wadau mbalimbali kutoa mwito kwa serikali kubuni, kujadili na kutekeleza sera pana ya pombe, itakayotumiwa kuzuia matatizo yanayoongezeka ya kiafya, kijamii na kiuchumi yanayotokana na matumizi ya vileo.

Kufuatana na hali ilivyo, Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) kimeanzisha mradi unaolenga kukabiliana na matumizi ya pombe kupita kiasi yanayochangia Ukatili wa Kijinsia (GBV).

TAMWA wamekutana na viongozi wa serikali za mitaa, wadau na makundi kwa mahojiano ili kupendekeza kata tatu za Makumbusho, Saranga na Wazo Hill, Wilaya ya Kinondoni kuhakikisha kuwa sera na sheria zinasaidia jitihada za kukabiliana na ulevi unaochangia GBV.

TAMWA iliingiza kwenye mradi huu baada ya kupokea mashauri ya ukatili kupitia kituo chake cha usuluhishi (Crisis Resolving Centre), na kubaini ongezeko la vitendo vya kutelekeza wanawake, ambapo katika kipindi cha miezi sita mwaka 2015, jumla ya mashauri 54 yalipokewa kituoni hapo.

TAMWA inaamini kwamba, kupitia mchango wake, wanaume watawajibika zaidi na kuacha matumizi yaliyopitiliza ya vileo, yanayochangia unyanyasaji wa kijinsia, na badala yake kuchangia ustawi wa familia na kukuza maendeleo kwenye jamii na katika taifa kwa ujumla. ▶▶ pg 5



Na Beatrice Bandawe

**A** NNA JOSEPH (sio jina lake halisi) ameamua kuondoka kwa mume wake kutokana na udhalilishaji aliokuwa akifanyiwa, na sasa anaitegemea biashara ya kuuza mboga, kula na kusomesha watoto wake wawili wanaosoma sekondari.

Ni mama wa watoto wanne, aliozaa na mume wake aliyefunga naye ndoa miaka 17 iliyopita.

Aliamua kuondoka na kumuachia nyumba kwa sababu ya manyanyaso na vipigo alivyokuwa akivipata toka kwa mume wake anaporudi nyumbani usiku huku amelewa, na kudiriki kumletea mwanamke mwingine ndani.

“Siku moja usiku nikiwa nimelala chumbani, mume wangu alikuja akiwa amelewa chakari na mwanamke, akaniamuru nitoke niwapishe... iliniuma sana,” anasema.

Anasema mume wake anafanyakazi ya ujenzi na anapata pesa nyingi, lakini yote inaishia kwenye pombe na wanawake.

Tukio la Anna ni kati ya matukio kadhaa ya ukatili wa kijinsia wanayofanyiwa wanawake kutokana na waume zao kunywa pombe kupita kiasi.

Anna, mkazi wa Kimara, alitoa ushuhuda huo baada ya Chama cha Wanahabari Wanawake (TAMWA), kufanya utafiti wa ukatili wa kijinsia unaosababishwa na pombe katika kata tatu za Wilaya ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam.

Kata zilizofanyiwa utafiti ni Saranga, Wazo na Makumbusho, ambako ukatili wa kijinsia (GBV), unaotakana na pombe umeonekana kushika kasi.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Saranga, John Njunde, ambaye anaongoza mitaa tisa ukiwamo wa Mji Mpya, Ukombozi,

# ‘Mume mlevi alinifanya niache nyumba yangu’



Mwanamke akisimulia mateso anayoyapata baada ya kupata kipigo kutoka kwa mumewe

Stop Over, Matangini, Kimara B, Upendo, King’ongo, Michungwani na Saranga, anasema matukio ya unyanyasaji wa aina hiyo

hayajawahi kuripotwa kwenye ofisi yake, lakini anachofahamu watu wa ustawi wa jamii ndio wanaopokea matukio kama hayo. ▶▶ pg 5

# Taifa linahitaji Sera ya Vileo haraka

« pg 3

Jamii yetu inatakiwa kupambana na athari mbaya kwa wengine zitokanazo na vileo, achilia mbali wanywaji – nazo ni kama ukatili kwa wanawake na watoto, kufuja fedha za kaya na ukosefu wa tija sehemu za kazi.

Matatizo yanayohusiana na utumiaji wa vileo kama vile yale ya afya ya akili na mwili yanatakiwa kupigwa vita, pamoja na uhusiano uliopo kati ya pombe na VVU/UKIMWI, ajali za barabarani na matatizo mengine ya kiafya na kijamii.

Kwa kuwa vileo huchochea umasikini na kubomoa usawa miongoni

mwa watu, ipo haja ya kuanzisha programu zitakazohakikisha kwamba wanawakehawaathiriki tena na ukatili baada ya waume wao kulewa pombe.

TAMWA inaona kwamba huu ni muda mwafaka kwa wadau mbalimbali kuunganisha nguvu na kuchangia uanzishwaji wa sera ya taifa ya vileo, ili kuzuia na kupunguza madhara yatokanayo na vileo kwa maendeleo za taifa.

Kuna haja pia kutazama mfumo na mbinu za sekta ya vileo nchini Tanzania, ambapo kampuni zinazotengeneza vileo hutumia mbinu nyingi na kubwa za masoko katika ushawishi ili kuwafikia wateja

wao, huku wakienda kinyume na kanuni zinazotakiwa kuzingatia hali halisi kwenye jamii.

Matumaini ni kwamba kampuni hizi hazitahujumu jitihada zinazolenga kupatikana kwa Sera ya taifa ya vileo, na kwamba Wabunge wataunga mkono na kutia msukumo kupatikana kwa Sera hii.

Ni matarajio ya TAMWA kuwa serikali itabuni Sera pana ya vileo haraka, ili kuzuia ongezeko la matatizo ya kiafya, kijamii na kiuchumi yanayosababishwa na matumizi ya pombe kupita kiasi. ■

## ‘Mume mlevi alinifanya niache nyumba yangu’

« pg 4

“Nikiwasemea ninaweza kujikuta nikipotosha takwimu hasa kwa kuzingatia kwamba mambo kama hayo katika jamii hayawezi kukosekana, isipokuwa siwezi kueleza kwa sababu sina uhakika na ukubwa wa tatizo, ninaweza kusema kuna matukio machache na kumbe ni mengi na ninaweza kusema ni mengi na kumbe yapo machache.”

Ofisa Ustawi wa Jamii Kata ya Saranga, Tabu Mshokela, akielezea hali hiyo, anasema matukio hayo yapo ingawa takwimu sahihi sio rahisi kupatikana.

“Ni ya kawaida tu ambayo yanatokana na baadhi ya wanaume kuendekeza starehe na kuacha wake zao. Yamekuwa yakiletwa ofisini kwangu na kusuluhishwa na mengine yamekuwa yakiishia huko kwenye serikali za mitaa ndiyo maana inakuwa vigumu kuweka takwimu sahihi,” anasema.

Hata hivyo, Mshokela, anakiri kukutana na kesi ngumu ambazo ameshindwa kuzipatia suluhu na kuamua kuzipeleka kwenye ofisi zao makao makuu.

Anasema kwa ujumla hakuna tukio kubwa la kudhuru mwili lililotokea kwenye eneo lake na kuongeza kuwa litakapokea, atalifikisha kwenye dawati la jinsia ili hatua zaidi za kisheria zichukuliwe.

Hata hivyo, Mshokela anasema inawezekana matukio hayo yakawepo kwenye mitaa mingine na kupelekwa kwa viongozi wa mitaa husika na likafika kwake kwa kuchelewa.

Mwenyekiti wa Mtaa wa King’ongo, Demetrius Mapesi, anasema matukio ya ukatili wa kijinsia mtaani kwake ni mengi hadi kufikia wanandoa kuvunjana miguu.

Anasema chanzo kikubwa cha tatizo hilo ni baadhi ya wanaume kujihusisha na uvutaji wa bangi, unywaji pombe na pia kuendekeza mapenzi nje ya ndoa.

“Wapo baadhi ya wanaume wamekuwa wakilalamikiwa na wake zao kwamba wakilewa huwa hawalali nyumbani na badala yake wanakwenda kwa vimada wao.”

Anasema kuwa hivi karibuni kuna wanandoa walitengana sababu

kubwa ikiwa ni hiyo pamoja na vipigo na manyanyaso mengine ndani ya ndoa yanayosababishwa na ulevi.

“Kuna kesi nyingi huwa zinafikishwa hapa ofisini, zile ambazo tunaona kwamba tunaweza kuzimaliza, huwa tunawakutanisha wahusika na kuwasuluhisha na kama zikiwa juu ya uwezo wetu tunazipeleka kwenye vyombo vya dola,” anasema.

Anafafanua kuwa matukio ya aina hiyo wakati mwingine hujitokeza hata mara 10 kwa mwezi, hali inayoonyesha kuwa vitendo vya ukatili wa kijinsia vinavyotokana na ulevi ni vingi vikiwamo, vipigo kwa wanawake na kutelekezwa na waume zao.

Mapesi anasema miaka ya nyuma aliwahi kuletewa kesi ya mwanaume kumvunja mguu mkewe katika ugomvi na kuamua kuifikisha kwenye vyombo vya dola, ingawa hajui nini kiliendelea baadaye.

Akingumzia vitendo hivyo kwenye mtaa wake, Mwenyekiti wa Mtaa wa Saranga, Godwin Muro, anasema anchokiona ni changamoto za kawaida ambazo husababishwa na ugomvi unaotokana na mambo makubwa mawili. ▶▶ pg 6

Anayataja mambo hayo kuwa ni baadhi ya wawanawake wanao olewa kuwa na umri mdogo. Anasema hali hiyo ya ugomvi inatokana na umri mdogo wa mwanamke ambao humsababisha kutojua mambo ya ndoa na kupelekea mikwaruzano na wenzi wao.

“Hili mimi ninalichukulia kama changamoto ya kawaida katika ndoa kwa sababu wanafika na kusuluhishwa, na wakati mwingine unakuta mwanaume ndiye anayekuja kumlalamikia mkewe.

Jambo la pili ni kwamba uchumi nao unachangia kusababisha migogoro ndani ya ndoa.

“Unaweza kukuta mwanaume uwezo wake kiuchumi ni mdogo, lakini mwanamke analazimisha kupewa vitu vya gharama kubwa na mwisho wa siku ugomvi unazuka kwamba mume hatoi matumizi nyumbani kwake na kumbe sababu ni hiyo” anasema.

Anaeleza kuwa mnamo mwezi julai 2016 ni matukio matatu yalikuwepo yaliyotokana na ulevi, kuongeza kuwa kuna changamoto ambazo ni vigumu kuzihesabu kwa sababu ni za kila mara ambazo huwa zishughulikiwa mara kwa mara.

Kwenye baadhi ya mitaa, ukiwamo wa Tegeta, Mwenyekiti wa serikali ya mtaa huo, Ahaba Lwiva, anasema kuanzia mwaka jana hadi sasa, wamepokea kesi moja ya unyanyasaji wa kijinsia.

Anasema kesi hiyo ilihusu mume kumnyanyasa kijinsia mke wake kutokana na ulevi, lakini walifanikiwa kuwasuluhisha na wanaendelea kuishi vizuri kwenye ndoa yao.

Hata hivyo, katika Mtaa wa Mabwepande, Kata ya Mabwepande, mwaka 2015 walipokea kesi 11, mwaka huu (2016) wamepokea kesi tatu.

Mwenyekiti wa Serikali wa Mtaa wa Mabwepande, Abdallah Kunja, anasema kesi hizo zilihusu ukatili wa kijinsia, hata hivyo, alishindwa

## ‘Mume mlevi alinifanya niache nyumba yangu’

kufafanua kama zilihusiana na ulevi kutokana na kukosa kumbukumbu.

Mtaa wa Bunju ‘B’ kuanzia mwaka jana hadi sasa, wamepokea kesi saba na nne kati ya hizo zimemalizika na wahusika wanaishi vizuri huku tatu zikiwa zinaendelea kupatiwa usuluhishi kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Serikali ya mtaa huo, Athuman Njama.

Kutokana na maoni ya wenyeviti hao, chanzo kikubwa cha kesi walizowahi kuzipokea ni ulevi, wivu wa mapenzi na kukosekana uaminifu katika ndoa. Vyanzo hivyo vya migogoro katika ndoa, kikubwa husababisha na wanaume kuendelea pombe na kusahau majukumu yao ndani ya familia.

Hata hivyo, wanasema kwa sasa kesi hizo zinapungua kutokana na wanandoa wengi kuwa na uelewa mkubwa wa masuala ya ukatili wa kijinsia katika ndoa.

Maelezo hayo yanatolewa na Ofisa Usuluhishi wa Dawati la Ustawi wa Jamii, katika Kata hiyo, Hellen Mtui.

Anasema aina ya kesi za ukatili wa kijinsia zilizoripotiwa ni wanawake kufukuzwa nyumbani na waume zao na kuwaacha watoto wadogo.

Aidha, wanawake kukimbiwa na wanaume zao na kuachiwa watoto.

Hellen anasema mengi ya matukio hayo husababishwa na ulevi wa wanaume au mwanaume kuwa na mwanawake mwingine (mchepuko). “Matukio haya ya mwanaume kuwa na mwanamke wa nje huchangiwa na unywaji pombe, mtu akishalewa anaanza kutamani mwanamke mwingine na hatimaye huanzisha mahusiano na kuzoana na matokeo yake mke ndani anaanza kukosa matunzo,” anasema.

Anasema sababu hizo huchangia wanaume kuanza kuwatesa wake zao, kuwanyima fedha za matumizi na kutosomesha watoto. “Wanaume

ambao ni walevikwakesi ninazopokea, hupiga wanawake, hukwepa kulipa gharama za matumizi ya nyumbani na kutosomesha watoto,” alisema.

Alisema sababu hiyo hufanya mwanamke kushindwa kumudu gharama za maisha na hivyo kuamua kuripoti polisi.

Aidha, anasema kwa mwanamke anaefukuzwa, hulazimika kuondoka na kuacha watoto wakiwa wadogo, na matokeo yake watoto hupata shida na wengine kwa sababu ya kukosa matunzo huishia kwenda mitaani na kuwa omba omba.

“Unakuta mama kafukuzwa, baba anabaki na watoto ambao wanahitaji uangalizi wa karibu wa mama, hivyo kusababisha watoto kukosa huduma muhimu na mwisho wa siku kuishia kuwa watoto wa mitaani,” anasema.

Mara nyingi kesi kama hizo, huripotiwa na wanawake ambao huzungumza nao na baadaye kuwaita wanaume ambao hukaa pamoja na kutafuta usuluhishi.

Anasema miongoni mwa kesi hizo ni chache zinazokwenda mahakamani. Hellen ambaye pia ni Katibu wa Baraza la Kata hiyo, anasema kesi tatu kati ya tano walizopokea mwaka 2016, wamepeleka mashauri yake Ustawi wa Jamii.

Alisema kesi nyingine mbili zimepeleka mahakamani kwa ajili ya kupeana talaka baada ya kushindwa kufikia muafaka kwenye ngazi yao.

“Kesi mbili kati ya hizo ilishindikana kuwasuluhisha wanandoa na hivyo wakaamua kuachana, na kesi hizo tulizipeleka makamani,” anafafanua Hellen.

Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971, ibara ya 7.1 inayongumzia haki za mwanamke katika ndoa, kifungu cha 66 kinakataza mwanandoa yeyote kumpiga mwenziwe kwa sababu yoyote ile. ■

# Ukweli halisi kuhusu vilabu vya usiku

Na Nelly Mtema



Msanii akitumbuiza katika Klabu ya usiku

**V**IJANA wengi, wanawake na watoto wamekuwa ni waathirika wakubwa wa athari za kisaikolojia hasa kutokana na kuishi jirani na baa za vilabu vya usiku ambazo nyingi si rasmi na ziko katika maeneo ya makazi ya watu.

Hali hiyo imepelekea vijana wengi kujiingiza katika ulevi katika umri mdogo kutokana na athari za mazingira ambapo mazingira ambayo yamekuwa ni kichocheo kikubwa cha hali hiyo.

Bi Irene Calistus, mkazi wa Kimara Stop Over jijini Dar es Salaam ameelezea athari wanazokumbana

nazo hasa kutokana na kuishi jirani na baa ya usiku.

“Unaamka asubuhi ukiwa unapeleka watoto shule unakutana na vijana wakiwa na wapenzi wao wanatoka kwenye hizo vilabu vya usiku, wamevaa nguo za ajabu na huku wakiwa wamelewa ambapo ufahamu wao wakati huo unaongozwa zaidi na ulevi” alisema

Aidha aliongeza kuwa inafika wakati wanajikuta wakitamani kujificha hasa kutokana na maswali ambayo watoto wamekuwa wakimuuliza ambayo kimaadili mzazi hupata wakati mgumu wa kumjibu.

Amedai kuwa vijana wengi wa maeneo hayo wamekuwa

wakiathirika kisaikolojia na wengi kujiingiza katika ulevi katika umri mdogo.

“Wazazi ambao tunaishi karibu na bar za usiku ambazo ziko katika makazi ya watu tuna changamoto nyingi za kimalezi na kimaadili ambapo taasisi husika inabidi kuingilia kati kwani wasipofanya hivyo, vizazi vijavyo vitakuwa na hulka na silka za ajabu” alishauri

Hilda Romeo (si jina halisi) ni mfanyakazi wa moja za bar za usiku zilizoko jijini Dar es Salaam katika manispaa ya Kinondoni ambapo amesema wamekuwa wakijikuta mara nyingi wakinyanyasika kijinsia hasa pale wateja wao wanakuwa wamelewa. ►► pg 8

“Ni ugumu tu wa maisha, lakini kiuhalisia ni kazi ngumu sana maana mara nyingi tunahudumia watu ambao wanatumia vilevi ambapo vikiwakolea hufanya mambo ya ajabu sana na wakati mwingine hukuacha na deni” alisema.

Zaidi ya hayo alisema wengi wamekuwa wakiwachukulia wahudumu wa kike wanaofanya kazi maeneo hayo kama wanafanya biashara ya kujiiza mwili hasa ikizingatiwa kuwa wengi wanaojihusisha na biashara hizo wamekuwa wakitumia maeneo ya baa za usiku.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo Cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Hellen-Kijo Bisimba alisema ni makosa kwa bar hizo kuwa katika makazi ya watu.

Alizilaumu serikali za mitaa na manispaa kwa kuruhusu baa hizo za usiku kujengwa katika makazi ya watu.

Amesema malalamiko ambayo yamekuwa wakiongezeka katika jamii kwamba vijana wengi wamekuwa wakijihusisha na ulevi unatokana na ukweli kwamba hakuna udhibiti wa kutosha kutoka mamlaka husika.

“Baa za usiku zilizo jengwa katika maeneo ya makazi ya watu, zimekuwa zikichangia sana katika kuporomoka kwa maadili kwani watoto na vijana wamekuwa wanajifunza kutoka katika mazingira yanayowazunguka na wanapokaa na vijana wenzao pia wanawashawishi kwa kuona kwamba ndiyo mfumo wa maisha” alisema Dk. Kijo Bisimba.

Baadhi ya wanafunzi walihojiwa wamesema kuwa wengi wamejikuta wakishindwa kujisomea wakiwepo nyumbani kwani bar nyingi za usiku zimekuwa zikipiga mziki kwa sauti kubwa na hivyo kuwafanya washindwe kuwa makini katika masomo yao hapo nyumbani.

Waliongeza kuwa kuna baadhi ya wenzao wamekuwa wakitoroka shule na kwenda kwenye baa hizo kucheza muziki na kujiingiza kwenye ulevi hali ambayo imekuwa ikiwafanya washuke kitaaluma.

# Ukweli halisi kuhusu vilabu vya usiku



“Bora mkuu wa mkoa wa Dar es Salaam alivyopiga marufuku watoto kuwa bar nyakati za usiku huenda ikasaidia ila kuna baadhi za bar za usiku ambazo hufanya kazi mchana zinatoa huduma mchana, na ndiko ambapo wanafunzi wengi wamekuwa wakienda” alisema mmoja wa mwanafunzi ambaye anaishi jirani na bar hizo.

Hali hii inajidhihirisha wazi katika utafiti uliofanywa na Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Shirika la Afya Duniani (WHO) umeonyesha kuwa asilimia saba ya vijana kati ya umri wa miaka 25-34 wanajihusisha na ulevi.

Mkuu wa Kitengo cha Afya ya akili na dawa za kulevya katika wizara ya afya, Dr Norman Sabuni amesema wizara imefanya utafiti juu ya athari za pombe hasa kwa vijana kati ta miaka 25 hadi 34 na kukuta asilimia saba wanatumia kilevi.

Alisema vijana wote wa kike na kiume, hasa wale wanaoishi jirani na bar na bar za usiku mbali na athari za kisaikolojia lakini pia wamekuwa wakijihusisha na matumizi ya pombe katika umri mdogo.

Amelaumu serikali za mitaa na halmashauri kwa kutoa leseni bila kujali athari za jamii husika.

Amesema sheria iliyopo ni ya mwaka 1968 ambayo haijadhhibiti mazingira ya uuzaji wa pombe bali imeweka muda wakuuza pombe na umri wa mtu kuweza kuuziwa pombe.

“Sheria inasema pombe itauzwa saa kumi jioni hadi saa sita usiku na iuzwe kwa mtu mwenye umri zaidi ya miaka 18, lakini ukiangalia serikali za mitaa na manispaa zimekuwa zikitoa leseni bila kujali mazingira” alisema Dr Sabuni

Amesisitiza haja ya kuifanyia marekebisho sheria hiyo vinginevyo itakuwa baadaye vigumu kudhibiti kwani vijana wengi watakuwa wanajihusisha na unywaji wa pombe.

“Unakuta mtu amefungua duka la kuuza bidhaa kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya nyumbani, halafu anaamua kuweka viti na kuanza kuuza vileo na baadae anaweka hapo na nyama choma, imeisha kuwa baa hiyo tayari bila kujali athari anazoleta kwa jamii husika.

Alisema pia athari za makelele zimekuwa ni kubwa mno kwa jamii inayozinguka baa hizo na hivyo wengi walilitaka Baraza la Taifa la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (NEMC) kuhakikisha wanashughulikia suala hilo.

Mwezi Machi 2016, NEMC ilitoa onyo kwa wamiliki wa baa, makanisa, kumbi za sherehe na club za usiku kuhusu makelele na kuwataka wadhhibiti kabla ya kuchukuliwa hatua husika.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Mhandisi Bonaventure Baya, amesema mamlaka yake imewatoza faini baadhi ya wamiliki ambao waliamua kukiuka sheria na kwamba hatua zaidi zitachukuliwa kwa wale watakaokiuka utekelezaji wa maagizo hayo. ▶▶ pg 9



# Ukweli halisi kuhusu vilabu vya usiku

« pg 8

Alizitaka baa na vilabu vya usiku ambazo ziko wazi kuhakikisha kuwa wanaweka mazingira na vifaa vitakavyozuia sauti kutoka nje na kuwapa usumbufu watu ambao wanaishi jirani na maeneo hayo.

Kumekuwa na malalamiko kutoka kwa jamii kwamba wamekuwa wakiathirika na kelele za bar na vilabu vingine vya usiku ambazo zimekuwa zikipiga muziki kwa sauti

kubwa na hivyo kuleta usumbufu kwa wananchi.

Mhandisi Baya amesema hivi karibu NEMC na kitengo cha police mazingira kitaanzisha msako maalum kuwakamata watu ambao wanasababisha usumbufu wa kelele kwa wananchi ili jamii ijenge utaratibu wa kujua haki zao na sehemu ya kwenda kupeleka malalamiko yao pale ambapo wanaona hawatendewi haki.

Kwa mujibu wa rekodi zilizopo mkoa wa Dar es Salaam una klabu za usiku ambazo ni rasmi zaidi ya 15 huku nyingi zikiwa si rasmi.

Mmoja wa wamiliki wa vilabu vya usiku ambaye hakutaja jina lake litajwe alisema ni vizuri manisipaa ikasimamia sheria na taratibu za uanzishwaji wa club hizo ili kuepuka athari.

“Mimi nikisema watasema nawachongea kwa sababu yangu imefuata vigezo, lakini udhibiti wa ulevi hasa kwa vijana ni ngumu kwani wengi ambao ukimuangalia unaona ni mwanafunzi huja na wapenzi wao na inakuwa ngumu kuingilia mahusiano ya watu” alisema.

Aliongeza kuwa “Ukiangalia unahisi kabisa Yule ni binti wa shule lakini kaja na mpenzi wake na tena anafundishwa kunywa bia kwa kumchanganyia na soda, lakini sasa unaanzaji, maana jibu utakalopewa, utasikitika na atakuharibia siku yako”.

Alidai kuwa awali alikuwa akiwashauri kuacha kuja klabu, kwani naye ni mzazi lakini amekuwa akipewa majibu ya kukatisha tamaa kwani kuna wakati binti mmjoka alimwambia “kama unajua kufuatilia maadili fungua klabu yako na usiuzie bia, acha kufuatilia maisha ya watu”.

Dr Sabuni alisema wizara inaanda sera ya unywaji pombe ambayo amesema kwa kiasi kikubwa itasaidia kutungwa kwa sheria ambazo zitadhibiti unywaji wa pombe na pia kuweka sheria na kanuni bora ni jinsi gani biashara hizo zierendeshwe kwa faida ya kizazi cha sasa na kijacho.

Alisema sera hiyo ambayo imepita katika ngazi ya wataalam inasubiri kupelekwa serikalini kabla ya kuwasilishwa kwa wadau ili watoe maoni hayo.

Hatua hii ni muhimu kwani nchi inahitaji sera ili kudhibiti unywaji na uuzwaji wa pombe na ujenzi wa bar na vilabu vya usiku katika maeneo ya makazi ya watu. ■

## Baa zinasababisha maadili kuporomoka

Na Jacks Meena

**U**dhaifu wa usimamizi wa mipango miji katika jiji la Dar es Salaam umepelekea ujenzi holela wa makazi ya watu, nyumba za biashara na mlundombinu duni.

Takwimu zinaonyesha kuwa jiji la Dar es Salaam lina zaidi ya wakazi wapatao milioni 6 na kila kukicha watu wanaoingia katika jiji hili ni wengi kuliko uwezo wa jiji kuwahudumia.

Kwa mantiki hiyo, Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake nchini (TAMWA) kimefanya utafiti na kubaini kuwa kutokana na kutokuwepo na mamlaka ya kusimamia huduma za mipango miji kumekuwepo na ukiukwaji mkubwa wa matumizi ya ardhi na majengo hususani katika wilaya za Kinondoni na Ubungo.

Mathalani, katika Wilaya ya Kinondoni kuna baa takribani 2,400 na kati ya hizo, 740 zipo katika Kata ya Sinza ambapo nyingi zipo katika maeneo ya makazi ya watu.

Uwepo wa baa hizi katika makazi ya watu umeleta athari nyingi kwa wakazi hao ikiwa ni pamoja na kuwaondolea utulivu unaohitajika katika maeneo waishio watu, maadili ya malezi ya watoto an vijana kuharibiwa, kuharibu mandhari na uchafuzi wa mazingira kwa ujumla.

“Ni kweli kuwa na baa kila pahala haipendezi maana tunapata shida kwa usumbufu wa makelele ya walevi na muziki. Vilevile uwepo wa baa hizi katika makazi ya watu kunachochea vitendo viovu kama vile uporaji, ukahaba, utumiaji wa madawa ya kulevya, unywaji wa pombe kupindukia hususan kwa wanafunzi wa shule ambao bado wanakuwa hawajawa na uelewa wa kutosha.” Anasema Bi. Jasmin Said (29), Mkazi wa Mji Mpya, Kata ya Saranga katika Wilaya mpya ya Ubungo.

Goodluck Mmari (53) ambaye ni mmiliki wa Bar maarufu ya Meeda katika eneo la Mori-Sinza anasema uholela wa bar hizo na grocery vingi unawakoshesha wamiliki wa baa ambazo zipo katika maeneo halali kama ya kwake ilivyo.

» pg 10

# Baa zinasababisha maadili kuporomoka

“Kama unavyoona katika eneo letu baa ni nyingi kila hatua tano au kumi unakutana na baa hivyo kupelekea biashara kuwa ngumu.

Lakini pia kumekuwa na ongezeko kubwa sana la dada poa wakati wa jioni,” anasema Bwana Mmari. Kuhusu uwepo wa matukio ya udhalilishaji wa kijinsia, Bwana Mmari anasema suala hilo ni gumu kubaini moja kwa moja kwa vile wateja hukubaliana na baada ya hapo inakuwa ngumu kujua.

Wakati Bwana Mmari akibainisha hayo, waendesha bodaboda katika eneo hilo wanasema udhalilishaji wa kijinsia kwa wanawake wanaojihusisha na bishara ya ngono na wapita njia ni kitu cha kawaida katika eneo hilo na baadhi ya wanaoume ambao huwapigia miluzi na kuwaita majina ya udhalilishaji kama vile vyura.

“Hivi majuzi kaka kama uliona kuna video ilisambazwa kwenye mitandao ya kijamii ikimuonyesha mwanamke

mmoja dada poa akifanyiwa kitendo cha ngono hadharani akiwa ameegemezwa kwenye taksi na yule aliyekuwa akifanya kitendo kile alikuwa anafurahia kitendo kile cha upigaji picha... na hakika baada ya picha ile kusambaa kwenye mitandao ya kijamii dada yule kwa namna moja au nyingine atakuwa anajihisi vibaya maana mambo yale yalipaswa kuwa ya siri,” anabainisha Bwana Kondo Mtumwa (28) mwendesha bodaboda.

▶▶ pg 11



Makampuni ya Bia yanatangaza vinywaji vyao maeneo ya baa. Swali la kujiuliza ni hili - Je makampuni haya yanajua madhara ya pombe kwa binadamu?

Boniface Mwaranda (38) ni mkazi wa Kibanda cha Mkaa katika kata ya Saranga, yeye anasema uwepo wa mabaa na nyumba za kulala wageni katika maeneo ya makazi haileti picha nzuri kwa wakazi wa maeneo husika maana ulevi na mambo ya ngono yanachochea maambukizi ya magonjwa kama vile ukimwi na magonjwa mengine ya zinaa.

“Hii bwana sio fresh kabisa hasa ukizingatia vijana wanaochipukia ni rahisi kuiga baadhi ya mambo haya na kuwaharibia maisha. Ukitembelea maeneo mengi ambako hizi baa zimezagaa utajionea mwenyewe maana hata wake zetu si salama kabisa,” anasisitiza Bwana Mwaranda.

Mwaranda anaendelea kubainisha kuwa siku za mwisho wa wiki hali huwa mbaya zaidi kwa kuwa walevi huwa ni wengi na hutoa lugha chafu sana na za kuudhi na wakati mwingine nyakati za usiku hujihusisha na vitendo vya uporaji hususan kwa wakina mama ambao huwa wanarudi majumbani baada ya shughuli zao za siku.

“Yaani ndugu wakati mwingine unamkuta jitu zima na heshima zake linaporomosha matusi mchana mzima huku watoto wakisikiliza matusi hayo. Wewe unadhani watoto wale watakuwa wanajifunza nini?” anahoji Mwaranda.

Akisimulia kisa cha kusikitisha kilichotokea katika baa moja katika Kata ya Saranga, Mwaranda anasema Mzee mmoja wa makamu (jina tunalihifadhi) aliamua kumdalisha mke wake hadharani kulikopelekea kuvuta umati mkubwa wa watu katika baa hiyo.

“Huyo Mzee inaonekana alimuhisi mke wake kuwa na mahusiano na mmoja wa madereva wanaopaki magari katika eneola baa yao. Sasa kwa mshangao wa wengi aliamua kumtolea mke wake wa ndoa lugha ya matusi tena kwa sauti akisisitiza kuwa kama dereva huyu anamwingilia kinyume na maumbile basi na yeye anaweza kuyafanya yote hayo,” anasimulia Mwaranda.

Anasema hali ile iliyotokea haikuwa fedheha tu kwa watoto wa mzee Sauti ya Siti

# Baa zinasababisha maadili kuporomoka



yule ambao walikuwepo bali kwa wanawake wengine mtaani pamoja na watoto kwa ujumla.

Diwani wa Kata ya Kibamba ambaye pia ni mwenyekiti wa madiwani wa jimbo la Kibamba, Bw. Ernest Mgawe (39), anasema uwepo wa baa katika maeneo ya makazi ya watu una athari kubwa kwa makuzi ya vijana hususan wa kike ambao hushawishiwa na wanywaji na kujikuta wakiingia katika vitendo vya ngono kabla ya umri wao.

“Unajua binti anapoitwa baa na mtu anayemfahamu ni rahisi kujiingiza katika mambo mengine maana jamaa ataanza kwa kumnunulia chipsi na soda na baada ya hapo inakuwa ni eneo la kupanga mambo mengine ambayo yatampoteza binti,” anasema Bw. Mgawe.

Mgawe anasema mbali ya kuchochea vitendo vya kingono, makele ya muziki huwa ni kero kubwa kwa wakazi wa eno husika ikiwa ni pamoja na vijana wa shule kushindwa kufuatilia mafunzo yao vizuri kutokana na usumbufu huo pamoja na matusi kutoka kwa walevi.

“Kwa kweli wanafunzi hawapati mazingira mazuri ya kujisomea maana kila pahala hugeuka kuwa kero. Ukweli kunakuwa hakuna utulivu kabisa,” anaongeza Bw. Mgawe.

Mzee Isakwisa Isaya (67), Balozi wa shina no.12 Mtaa wa Mji Mpya, kata ya Saranga-Temboni, anasema uwepo wa baa na nyumba za kulala wageni katika maeneo ya makazi ya watu ni kero kubwa kwa wakazi wa maeneo hayo maana baa hizo huleta watu kutoka sehemu mbalimbali na wenye tabia tofauti hivyo kuharibu maadili na taratibu za wakazi wa eneo husika.

Mathalani katika eneo lake ambapo kuna maduka matano yanayouza bidhaa za nyumbani huwa yanauza pia vilevi, pamoja na kwamba kuna nyumba moja ya kulala wageni na hii ni hatari kwa usalama wa raia na mali zao.

“Unajua mwanangu hivi vitu huvutia watu wa aina mbalimbali sasa katika mchanganyiko huo wahalifu nao wapo, watu wa michepuko nao wamo hivyo katika mseto huo vitendo vya udhalilishaji kwa akina mama na wasichana haviwezi kukosekana,” anasema Mzee Isaya.

Naye Meya wa Manispaa ya Kinondoni Bwana Boniface Jacob anatambua changamoto hiyo na kwamba Manispaa yake imejipanga kuzirekebisha katika mpango mkakati wa kuiweka Manispaa ya Kinondoni katika mpangilio wa kisasa.

“Kama unavyofahamu kulikuwa na udhaifu katika kusimamia mambo haya lakini sasa tumeingia kwa mtazamo mpya na hakika tutasimamia na kuhakikisha kasoro hizi tunaziondoa haraka iwezekanavyo,” anasema Bw. Jacob.

Anaendelea kubainisha kuwa Manispaa yake imejipanga kutekeleza kauli ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Bw. Paul Makonda aliyeitoa wakati akiwa Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni ambapo alipanga kuwepo kwa eneo maalumu kwa ajili ya shughuli za baa tu. ■



# Utitiri wa baa jijini: Je serikali inapata kodi stahiki?



Rais John Pombe Magufuli anasisitiza kuwa makampuni na watu binafsi ni lazima kulipa kodi staiki

Na Chabby Barasa

**H**uku baa zikiendelea kuchipuka kama uyoga jijini Dar es salaam kila kukicha, kumekuwa na mashaka kutoka kwa baadhi ya watu iwapo serikali inapata kodi yake kama inavyostahili.

“Kasi ya kuibuka kwa baa, nyingi zikiwa karibu karibu inamaana kuwa hii ni biashara yenye faida kubwa,” anasema mzee Ben Malangalila, mfanyakazi mstaafu katika sekta ya umma, ambaye anaeleza wasiwasi wake kama baa zote hizo zinalipa kodi inavyotakiwa.

Mzee Malangalila anawapa changamoto Mamlaka ya Mapato Tanzania-TRA, kufanya kampeni maalum kuwakamata wamiliki wa

baa ambao watabainika kutolipa kodi kama inavyostahili, na hivyo kupunguza uwezo wa serikali kutoa huduma kwa watu wake.

“Tunawezaje kutegemea serikali ijenge barabara mpya, shule na hospitali kama miongoni mwetu wapo wasiolipa kodi?” anahoji Mzee Malangalila.

Maoni hayo yanaungwa mkono na mwandishi mwandamizi Anthony Tambwe, ambaye anasema kuwa baadhi ya baa zinaendeshwa katika mfumo usio rasmi na wa kisiri hivyo wahusika si rahisi kutambua uwepo wao.

“Kuna baadhi ya baa jijini Dar es Salaam amabzo hazina hata majina lakini zinasheheni wateja kila siku, zikiwahakikishia wamiliki kipato cha uhakika ambacho sehemu yake ilitakiwa iende serikalini kama kodi

ili kuboresha huduma za jamii,” anasema.

Kwa upande wake, Maimuna Semzigi, wasiwasi wake sio tu kama baa zinalipa au hazilipi kodi, isipokuwa suala ni sehemu zilipo, kwani baadhi zipo jirani mno na shule, nyumba za ibada na vituo vya afya.

“Hakika hakuna ulazima wa kuwa na baa nyingi katika maeneo yetu, hata kama zinalipa kodi na kufanya biashara kihalali,” anasema Bi Semzigi, mkazi wa Sinza Madukani jijini Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa Maimuna, miaka ya nyuma Sinza ndio ilikuwa kinara wa kuwa na baa nyingi katika eneo moja, lakini sasa maeneo mengine kama Tabata na Kinondoni yamefuata mkumbo huo. ▶▶ pg 13



# Changamoto zinazowakumba wahudumu wa baa Dar

Na Anthony Tambwe

**K**unywa pombe na marafiki huku mkifurahia hiki na kile ni jambo la kawaida katika maeneo mengi ya baa jijini Dar es Salaam, lakini katika maeneo hayo kuna watu wanaoteseka kimya kimya.

Kwa wale wapenzi wa bia, kuipata yenye ubaridi ni jambo la kufurahisha, na ukimaliza hiyo kumwita mhudumu akuletee nyingine ni jambo la kheri pia.

Watu wanaotumika zaidi kutoa huduma hii ni akina dada ambao wanajulikana zaidi kama baameidi ambao kwa namna moja au nyingine wanapitia magumu ya aina mbalimbali kutoka kwa wateja wao.

Ni hizi changamoto ambazo zimekifanya chama cha waandishi habari wanawake Tanzania (TAMWA) kuanza kampeni za kuona ni kwa jinsi gani jamii inaathirika na unywaji pombe, na hasa kunyanyaswa kwa kina dada ambao wanatoa huduma kwa wateja.

Uchunguzi wa TAMWA uliofanywa hivi karibuni umeonyesha kuwa akina dada wanaohudumu maeneo mengi ya baa jijini Dar es Salaam wamekuwa wakifanyiwa vitendo vya udhalilishaji ambavyo ni kinyume cha sheria

Jambo ambalo wengi hatujui ni ukweli kwamba wengi wa hawa kinadada, wengine wakiwa miaka kumi na nne hawaridhishwi na matendo hayo, na wanatamani serikali iweke sheria ya kuwaadhibu wale wote ambao wanawadhalilisha.

“Kunyanyaswa kijinsia katika maeneo yetu ya kazi ni jambo la kawaida kila

siku. Wateja wetu wengi wakishalewa wanapenda kututomasa kokote wanakotaka, na cha kushangaza hawataki tuwapinge uamuzi wao” anasema Amina anayehudumu baa moja iliyopo maeneo ya Tegeta.

Anasema kuwa muda mwingi anapohudumu baa anakumbana na changamoto za aina mbalimbali, cha kuhuzunisha zaidi ni unyanyasaji wa kingono ambao anakumbana nao.

“Kwa vile tunauza vileo ambavyo vinafanya wateja wetu kulewa na kufanya mambo ya ajabu tunateseka sana. Wengi wao wakishalewa wanashindwa kujizuia na kufanya mambo ya ajabu” anasema.

Alipoulizwa kwa nini huwa taarifa ya mambo hayo kwa vyombo vya kisheria, dada huyo anasema ni kwa vile wengi ya waathirika ni wasichana wadogo kutoka maeneo ya vijijini ambao wanaogopa kupoteza ajira yao.

Kwa bahati mbaya wenye mabaa hawaoni ubaya wa wafanyakazi

wao kutomaswa bila ridhaa yao na wapo baadhi yao wanaowaruhusu wateja wao kuwafanyia vitendo vya udhalilishaji wafanyakazi hawa.

“Waajiri ambao hawachukui hatua kuzuia wafanyakazi wao kudhalilishwa wanaweza kujisababishia gharama kubwa kutokana na kupungua kwa mauzo, morali ya kazi kupungua, kuchelewa kazini” anasema bwana Nelson Samson ambaye ni mwanasheria anayeishi maeneo ya Tegeta Dar es Salaam.

Anasema Sheria ya Ajira inamtaka kila mwajiri kupinga vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia maeneo ya kazi. Sheria inamtaka mwajiri aonyeshe ni kwa namna gani anapinga unyanyasaji wa kijinsia katika eneo lake la kazi.

Anaongeza kusema kuwa sheria inatamka wazi kuwa mteja yeyote anayemdhaliisha mhudumu anastahili kupata adhabu kwa mujibu wa sheria ikiwa ni pamoja na mhusika kupelekwa mahakamani. ▶▶ pg 15



Pombe ya miwa inawaathiri sana watu wengi maeneo ya vijijini.



# Utitiri wa baa jijini: Je serikali inapata kodi stahiki?



◀ pg 12

Uwepo wa baa nyingi unaendana na ripoti iliyotolewa hivi karibuni, ikisema Tanzania ni moja ya soko la bia lenye faida kubwa kabisa barani Afrika, kwa mujibu wa utendaji wa Kampuni ya Bia nchini –TBL, ambayo inahodhi takribani asilimia 75 ya soko la ndani.

Ripoti hiyo iliyotolewa na kampuni ya BMI Research ya Uingereza mwaka jana inatoa picha kuwa Tanzania itaendelea kuwa soko la bia lenye faida kubwa hadi mwaka 2019.

Ripoti hiyo ilithibitisha kuwa mauzo ya bia na kodi yake yataendelea kutoa mchango mkubwa kwa uchumi wa nchi, kama ambavyo takwimu za hivi karibuni zilivyoonyesha kuwa sekta ya vileo ilichangia hazina zaidi ya shilingi trilioni nne katika kipindi cha miaka kumi iliyopita.

Hata hivyo, huku kukiwa na mashaka juu ya ulipaji kodi wa baa hapa jijini, meneja wa baa ya Rose Garden ambaye alijitambulisha kwa jina moja tu kama Juma, alisema hawezi kuzungumzia baa nyingine, lakini alisisitiza kuwa baa yake imekuwa ikilipa kodi kama inavyotakiwa.

“Kama unavyoona tunatumia mashine za kielektroniki za EFD kutoa bili kwa wateja,” alisema na kuongeza kuwa Rose Garden inaona fahari kulipa kodi kama inavyotakiwa na hivyo kuunga mkono uchumi wa nchi.

Utaratibu wa kutumia mashine za EFD kutoa bili kwa wateja pia unafanyika katika baa ya London Pub na Mabibo External jijini Dar es Salaam.

“Matumizi ya mashine ya EFD, mbali ya kuihakikishia serikali mapato yake, pia inaniwezesha kufuatilia mauzo kwa urahisi,” anasema meneja wa baa hiyo ambaye hata hivyo hakupenda jina lake litajwe.

Akizungumzia ulipaji wa kodi kwa baa, Mkurugenzi wa Elimu na Huduma kwa Mlipa Kodi wa TRA, Richard Kayombo anasema Mamlaka imeweka mikakati kuhakikisha baa zinalipa kodi kama inavyotakiwa.

Bw. Kayombo anaongeza kuwa kutokana na ukweli kuwa baadhi ya baa tayari zinatumia mashine za EFD inamaanisha kuwa utaratibu unafuatwa na serikali inapata mapato yake.

Anaeleza kuwa baa, kama ilivyo kwa biashara nyingine zinazotumia mashine za EFD kwa sasa ni zile ambazo mauzo-ghafi yake kwa mwaka yanafikia shilingi milioni 14 na zaidi.

“TRA muda wote ipo macho ili kuwabaini wafanyabiashara wasiolipa kodi, na Mamlaka haitasita kuwachukulia hatua wote wanaokwenda kinyume cha utaratibu,” anasema.

Anabainisha zaidi kuwa TRA inafikiria mpango ambapo kila ofisa wake atapangiwa eneo maalum la kusimamia kuhakikisha kila mfanyabiashara anaetakiwa kutumia mashine ya EFD au vinginevyo analipa kodi kama inavyostahili.

Jitihada za Mamlaka ya Mapato zinaendelea ili kupambana na ukwepaji wa kodi na kuziba mianya iliyopo, kuongeza vyanzo vya mapato na kusisitiza matumizi ya mashine za EFD ili kuongeza kasi ya ukusanyaji mapato.

Baa na migahawa imejumuishwa katika utekelezaji wa awamu ya pili ya matumizi ya mashine za EFD, lengo likiwa ni kuongeza idadi ya wafanyabiashara wanaotumia mashine hizo kutoa risiti katika kila muamala wanaofanya.

Kwa mujibu wa tangazo la TRA, mfumo huo ni endelevu na taratibu, mamlaka itaweza kusajili wafanyabiashara, ikijumuisha baa, kutegemeana na utendaji kibiashara.

Bw. Kayombo anasema matumizi ya mashine za EFD kwa baa yanaendana na juhudi za serikali kuhakikisha matumizi kamilifu ya mashine za EFD katika makusanyo ya mapato.

“Hakika hili ni moja ya maeneo ambayo serikali ya awamu ya tano imeyapa kipaumbele kutekeleza dhamira yake ya kuongeza na kuimarisha makusanyo ya mapato ya ndani,” anaeleza.

Hata hivyo, ili jitihada za serikali za kukusanya mapato ziwe na manufaa zaidi, taasisi mbalimbali kama Chama cha Wanahabari Wanawake nchini –TAMWA kimekuwa kikitoa hamasa kwa serikali kuhakikisha kuwa kipaumbele cha bajeti kinakuwa katika maeneo ya huduma muhimu kama vile elimu, maji na afya.

Maeneo hayo yanatajwa na TAMWA kuwa ni muhimu ili kukabiliana na umaskini hususani maeneo ya vijijini ambako ndiko wananchi wengi wanaishi kwa sasa kwa mujibu wa takwimu zilizo.

Kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya pombe, TAMWA pia ipo katika mkakati wa kuelimisha jamii dhidi ya unywaji pombe uliopita kiasi ili kukomesha ukatili wa kijinsia ambao utafiti uliofanywa hivi karibuni ulionesha kusababishwa na ulevi uliopindukia. ▶▶ pg 15



## Utitiri wa baa jijini: Je serikali inapata kodi stahiki?

◀ pg 14

Akisoma bajeti ya Mwaka wa Fedha 2016/17 hivi karibuni, Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt. Phillip Mpango alisema kuwa matumizi ya mashine za EFD yanatarajiwa kuongeza ufanisi na kupunguza upotevu wa mapato.

Mh. Waziri pia alizungumzia mipango mbalimbali ya TRA ya kuboresha makusanyo ya mapato na kupanua wigo wa kodi. Mapendekezo hayo yanajumuisha; kuweka kumbukumbu na taarifa sahihi za walipa kodi, kuhakikisha kuwa walipa kodi walioandikishwa kama vile wamiliki wa baa wanapewa mashine za EFD na pia wanazitumia kikamilifu katika miamala yao; kuimarisha ukaguzi wa taarifa za walipa kodi na kutengeneza mfumo wa taarifa sahihi kuhakikisha malengo yaliyowekwa ya makusanyo ya kodi yanatimia; kuanzisha vitengo vya EFD katika mikoa ya TRA jijini Dar es Salaam na vituo vipya vya huduma kwa walipakodi ili kuongeza makusanyo.

Kwa mujibu wa bajeti ya Mwaka wa Fedha 2016/17, serikali imejielekeza zaidi katika kuboresha miundo mbinu ya kuboresha huduma za maji, umeme na usafirishaji kwa ajili ya maendeleo ya uchumi wa viwanda na pia kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo ambayo yanatumika kama malighafi viwandani.

Kwa upande mwingine, ili kutimiza lengo la serikali, wachambuzi wanatoa rai kwamba mkazo uwekwe katika kuboresha makusanyo ya mapato ya ndani, kama vile kutoka baa na vyanzo vingine vikubwa vya mapato na kutenga mapato kuendeleza maeneo muhimu kuvutia uwekezaji wa kiviwanda. ■

## Changamoto zinazowakumba wahudumu wa baa Dar

◀ pg 13

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, Bi Helen Kijo-Bisimba, anasema kuwa kufanya kazi maeneo ya baa ni kama kwenye ajira nyingine yoyote ile, kwa hiyo kina dada wanaofanya kazi maeneo hayo inabidi waheshimiwe na kutendewa kama wafanyakazi wengine wowote wale.

Anasema kuwa tatizo ni kuwa baa nyingi hazina makubaliano ya kikazi na hawa baamedi, na hii ndio inawafanya kutotoa taarifa wanapokumbana na unyanyasaji wa kijinsia kwa sababu ya uoga wa kupoteza kazi.

Bi Kijo-Bisimba anasema kuwa kufanya kazi baa ni sawasawa na walimu wanaofundisha mashuleni kwa sababu wanatoa huduma kwa jamii jivyo ni wajibu wa waajiri wao kutunza haki zao za kimsingi kama binadamu.

“Kulinda haki za kibinadamu ni muhimu kwa makundi yaliyopo katika mazingira hatarishi ambapo mara kwa mara hunyanyaswa kwa namna moja au nyingine. Wanaoishi katika kundi hili wanapaswa wajengewe uwezo wa kuweza kuwashtaki wale wanaodhalilisha. Jamii ikiweka mkazo katika hili itasaidia sana” anasema.

Ukitembelea maeneo mengi yenye baa jijini Dar es Salaam utagundua kuwa unyanyasaji wa kijinsia unaendelea katika maeneo hayo kiasi kwamba yanaanza kuzoeleka kama mambo ya kawaida na hali hii ndio inapaswa kushughulikiwa na jamii kwa ujumla ili kukomesha tabia hiyo.

Dada Jane Mushi ambaye ni baamedia maeneo ya Tegeta anasema kuwa sio kweli wahudumu wanawawinda wanaume za watu, kwani yeye anasema huwa hana tabia hizo na kinachomfanya afanya kazi hiyo ni mshahara ili aweae kuendesha maisha yake bila shida.

Anasema kuwa akipata kazi nyingine yenye maslahi zaidi atakuwa tayari kuifanya na kuacha kazi ya baamedi.

Hata hivyo Mushi anakiri kuwa sio baa zote ambazo baamedi wananyanyaswa, kwani kuna maeneo mengine wanaheshimika na kufanya kazi zao bila manyanyaso yoyote.

Mtetezi wa Haki za Binadamu aitwae Daima Komboh anasema kuwa wahudumu wa baa inawabidi kuwa wavumilivu ili kulinda ajira zao, wasikubali kucheze maeneo fulani ya miili yao ili kuendelea kufanya kazi katika eneo husika.

Kunasheria zinazomlinda mfanyakazi lakini hazitekelezwi maeneo ya baa, kwani tofauti na maeneo mengine ambapo unyanyasaji wa kijinsia ni kosa kubwa, maeneo ya baa sheria bado haijachukua mkondo wake na kuwaadhibu wote wote wanaonyanyasa wanawake wanaohudumu katika baa nyingi jijini.

“Wengi wa wasichana hawa wanakubali manyanyaso kwa sababu hawaijui sheria. Wasichokijua ni kuwa wanaweza kupeleka malalamiko yao kwa vyombo husika na wahusika wakapewa adhabu stahiki” Anasema.

Helena Lihawa anasema kuwa wahudumu wa baa ni miongoni ya wanawake ambao wamekuwa wakinyanyaswa kwa njia mbalimbali.

Hii ndio inawafanya baadhi ya hawa wahudumu kuacha kuripoti kwa vyombo husika tabia sa unyanyasaji wa kijinsia wanavyofanyiwa na wateja wao.

Juhudi zinazofanywa na TAMWA zinaweza kupunguza magumu wanayopambana nayo kwa vile wahudumu wengi wa baa hawajui sheria inasema nini kuhusu haki za msingi. ■



# Sera ya Vileo inahitajika kuthibiti unywaji holela

Na Abdallah Msuya

**M**atumizi ya pombe na athari zake ni tatizo linalozidi kukua nchini Tanzania, na linapaswa kudhibitiwa haraka iwezekanavyo, wanaonya maofisa wa afya.

Ripoti ya Hali ya Pombe na Afya iliyotolewa na Shirika la Afya Duniani (WHO) mwaka 2014 inaonyesha kwamba asilimia 34 ya watanzania wanakunywa pombe.

Ripoti hiyo inasema kuwa asilimia 40.6 ya Watanzania wenye umri kuanzia miaka 15 kwenda juu wamekuwa wakijiingiza kwenye

tabia ya kunywa pombe kila siku katika maisha yao, japo kiwango cha kunywa kinatofautiana.

Ripoti inadai kuwa ongezeko hilo linawahusu watoto wa kiume na wa kike ambao wanajiingiza kagatika tabia hizo bila kujua ahari mbaya zinazoweza kuwaathiri kiafaya.

Kinachoogopesha zaidi ni kuwa watanzania wengi wa umri huo wanakunywa pombe za kienyeji ambazo hazijapimwa na taasisi kama ile ya chakula na dawa (TFDA) jambo ambalo linawaweka watumiajio hao katika athari kubwa katika maisha yao.

Ripoti ya Shirika la Afya Duniani (WHO) inaonyesha kuwa pombe zilizoidhinishwa na vyombo husika zinapatikana mijini zaidi, huku wakazi wa vijijini wakiendelea kunywa pombe za kienyeji asilimia yake ya ulevi kwa lita moja haijulikani.

Mkuu wa kitengo cha Afya ya Akili na madawa ya kulevya katika Wizara ya Afya, Jamii, Maendeleo, Jinsia, Wazee na Watoto, Daktari Norman Sabuni anasema kuwa idadi ya wanawake Tanzania wanaokunywa pombe ni asilimia 7.4, wakati wanaume ni asilimia 23. ▶▶ pg 17



Ajali nyingi zinazotokea nchini zinasababishwa na unywaji pombe





# Sera ya Vileo inahitajika kuthibiti unywaji holela

« pg 16

Utafiti uliofanywa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii mwaka 2013 unaeleza kuwa idadi ya wanaume wanaokunywa pombe Tanzania kupita kiasi ni milioni tatu na nusu, na wanawake ni milioni na laki saba.

Utafiti huo unaonyesha kuwa asilimia 30 ya vijana wa kitanzania vijana wenye umri chini miaka 15 na kuendelea hunywa pombe au wanatumia madawa ya kulevya, na sababu kubwa ya wao kunywa inahusishwa na uuzaji wa pombe katika maeneo wanayoishi.

Ongezeko hili la unywaji pombe katika jamii ya watanzania linavitaka taasisi husika pamoja na serikali kuangalia kwa haraka namna ya kudhibiti tabia hiyo na kunusuru maisha ya vijana yanayoendelea kuharibika kila kukicha.

Kwa mujibu wa Daktari Kissah Mwambene ambaye ni Katibu Mkuu wa Chama cha Madaktari wa Afya ya Akili Tanzania (MEHATA), mgonjwa mengi ya akili husababishwa na matumizi ya kupindukia ya pombe, ambayo hugarimu taifa pesa nyingi kuwatibu waathirika.

Anasema kuwa kuna madhara makubwa ya kiuchumi na na kiafya yatokanayo na matumizi mabaya ya pombe, na bahati mbaya wanawake na watoto ndio makundi yanayoathirika zaidi, hali inayotaka kuwepo na mikakati mahsusi ya kushughulikia jambo hili.

Dk. Mwambene anasema kuna watu wengi wanaokunywa pombe kupita kiasi, na hivo kuathirika kiuchumi na kiafya.

“Kumekuwepo na ongozeko la unywaji pombe ambalo husababisha vurugu katika jamii, na hasa maeneo ambapo kuna mfumo dume, na hivyo kuwafanya wanawake kupata matatizo ya kisaikolojia na kijamii” anasema.

Anaendelea kusema kuwa unywaji pombe kupita kiasi huchochea kuongezeka kwa kasi kwa matatizo mengine kama vile maambukizi ya ukimwi, kujiua, kujeruhiwa na hata kifo.

“Kunywa pombe kupita kiasi huchangia migogoro ya familia, ongezeko la talaka, kutokufuata uzazi wa mpango na pia kuongezeka kwa idadi ya watoto wa mitaani” anasema Dk Mwambene.

Anaongeza kuwa kuna watu wengi zaidi wanajiua na hii imeifanya Tanzania kuwa nchi ya nane barani Afrika ambapo watu wanajiua kwa sababu mbalimbali ikiwepo ulevi wa kupindukia.

Anaonya kuwa vijana wako katika hatari kubwa kwa sababu kuna uwezekano wa ubongo wao kuathiriwa na mwishoni wakaishia kuwa vichaa.

Mazingira magumu ambapo wanawake wanaishi yanaweza kuwafanya kunywa pombe na hivyo kuwaathiri na hasa wakati ni wajawzito, na hii inaweza kuwafanya kuzaa watoto ambao afya zao ni dhaifu, wakaishi muda mfupi na kufariki.

Kwa mujibu wa Dk Mwambene, wanawake ambao hunywa wakati ni wajawazito huweza kuongeza hatari ya wao pia kupata matatizo makubwa ya kiafya yatakayo waathiri baadae.

“Katika vyuo vyetu vikuu nchini tuna vijana ambao wamekuwa walevi hali iliyowasababisha kukatisha masomo yao. Vijana hawa wakirudi vijijini wanaendelea kuwa mzigo kwa taifa na wengine hugeukia wizi na ukahaba ili waweze kupata kipato” anasema.

Matatizo ya afya ya muda mrefu yanayohusishwa na matumizi hatari ya pombe ni pamoja na uharibifu wa ini, moyo, na hata kuongezeka kwa uwekano wa kuugua saratani, inabainisha Dr Mwambene.

Kumekuwepo na mkakati wa kimataifa wa kupunguza unywaji pombe unaosababisha madhara mabaya kwa mtumiaji na aache kujishughulisha na mambo yanayomletea kipato chake cha kila siku.

Mtaalam mwingine wa afya Daktari Shaibu Mashombo anasema kuwa watu wengi wamekuwa wakinywa pombe bila kujua athari zake na wanapoanza kuugua magonjwa yanayosababishwa na ulevi wanaanza kujuta.

Dr Mwambene anasema uundaji na utekelezaji wa sera kali kuhusu matumizi ya pombe ni jukumu muhimu katika kupunguza uharibifu unaosababishwa na matumizi mabaya ya vilevi mbalimbali.

Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo hazijabuni na kutekeleza sera ya pombe kitaifa na hii inapaswa kufanyiwa kazi haraka ili kupunguza athari za pombe katika jamii na kulifanya taifa kuwa na mwelekeo sahihi kuhusiana na mambo yanayohusu vilevi mbalimbali.

“Tunahitaji kuhakikisha kuwa tuna sera ya kitaifa ya pombe na ianze kutekelezwa mapema iwezekanavyo. Ni lazima tuwe na mpango shirikishio ambao utaisaidia jamii yetu” anasema.

Dr Mwambene anapendekeza lupitiwa kwa sheria na kuwekwa kwa masharti kuhusiana na matangazo, uuzaji na udhamini wa pombe pamoja na kuonyeshwa kwa onyo la athari za pombekwenye matangazo ya vilevi ili kupunguza matumizi yake kwa jamii.

Wabunge nao wamekuwa mstari wa mbele kuunga mkono kuwepo kwa sera hii ya matumizi ya pombe ili watanzania kwa ujumla waweze kunywa kwa kiasi kilichokubalika na sio kujiingiza katika ulevi ambao unaathiri maisha yao ya kila siku.

Mbunge wa Songea mjini Bwana Leonidas Gama anaishauri serikali kutunga sera madhubuti ya udhibiti wa pombe katika jamii ili pamoja na mambo mengine kuhakikisha vijana wanalindwa dhidi ya bidhaa hiyo.

» pg 19

Na Ashery Mkama

**K**wa muda mrefu, ajali za barabarani zimeendelea kuwa chanzo kikuu cha ulemavu wa kudumu na vifo miongoni mwa watu wenye umri wa miaka 10 – 50 katika nchi nyingi zinazoendelea, ikiwemo Tanzania.

Ajali za barabarani ni tatizo kubwa la afya kwa dunia nzima na inakadiriwa kuwa watu 3,000 hadi 30,000 wanajeruhiwa vibaya kutokana na ajali za barabarani kila siku duniani na sehemu kubwa ya ajali hizo zikiwa zinatokea katika nchi za uchumi wa chini na wa kati.

Ajali ya hivi karibuni iliyohusisha mabasi mawili ya kampuni ya City Boy yaliyogongana uso kwa uso katika eneo la barabara ya Maweni-Kintinku katika wilaya ya Manyoni, mkoa wa Singida ambayo ilisababisha watu takribani 30 kupoteza maisha na wengine wengi kujeruhiwa.

Hii imepelekea serikali kuja na sheria kali kwa lengo la kukabili tatizo la ajali za barabarani, na Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa alinukuliwa akiwaagiza mamlaka ya usafiri wa majini na nchi kavu (SUMATRA) kutunga sheria kali ambazo zitasaidia kukomesha tatizo la ajali za barabarani.

“Ni dhahiri kwamba sheria zilizopo hazina nguvu ya kutosha kupeleka ujumbe unaotakiwa kwa madereva wazembe na wamiliki wa mabasi. Sasa ni wakati muafaka wa kuweka sheria kali zaidi kukabiliana na tatizo hili,” waziri Mbarawa alisisitiza.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Kikosi cha usalama barabarani nchini, DCP Mohammed Mpinga, jumla ya watu 1,580 walikufa kutokana na ajali za barabarani katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Juni 2016. Pia ndani ya kipindi hicho jumla ya ajali 5,152 zilitokea na kujeruhi watu 4,659.

# Ulevi unachangia ajali za barabarani



Polisi akichukua vipimo kujua kama dereva wa basi amekunywa pombe

DCP Mpinga alielezea kwamba adhabu inayotolewa kwa madereva wanaotumia pombe ni kuwakamata pamoja na magari yao na kutowaruhusu kuendesha. Hatua ya pili ni kuwatoza faini ya shilingi 30,000/- au kuwashtaki mahakamani.

“Mara nyingi kama dereva akisababisha ajali akiwa amelewa tulikuwa hatumtozi faini bali tunajumuisha kosa lake na ile ajali mahakamani. Adhabu zinazotolewa kwa madereva wa aina hiyo hazitoshelezi kupunguza ajali na kukomesha tabia ya madereva wanaoendesha wakiwa wamelewa, faini ya 30000/- na kushitakiwa mahakamani pekee haitoshi” Alisema DCP Mpinga.

Kwa mujibu wa Sheria ya usalama barabarani Ibara ya 168 ya mwaka 2002 kifungo namba 44 mtu

anayepatikana na hatia atatozwa faini ya kuanzia 15,000/- lakini isiyozidi 50,000/- au kifungo cha miaka isiyopungua miwili na isiyozidi mitatu.

Alisema hukumu zinaweza kurefushwa kwa sababu faini ni ndogo na licha ya kuwepo kwenye sheria hukumu ya kifungo, bado hakuna dereva aliyewahi kufungwa.

“Ninapenda kuwashauri madereva wote wazingatie mafunzo waliyopewa katika vyuo vya udereva ambako walifundishwa pamoja na mambo mengine, madhara ya kutumia pombe wakati wanapotumia vyombo vya moto. Na muhimu zaidi, kama mtu ameenda kulewa basi awe na dereva mwenzake ambaye ataendesha gari lake au taksi kumrudisha nyumbani akitokea kwenye kumbi za starehe” anasema. ▶▶ pg 19

# Ulevi unachangia ajali za barabarani

« pg 18

Anasitiza kuwa ni muhimu madereva wetu wazingatie mafundisho ya dini zote yanayokataza ulevi. Kwa upande wa takwimu, katika kipindi cha miezi sita kuanzia Januari hadi Juni, 2015 ajali zilizosababishwa na pombe zilikuwa 34 na katika kipindi hicho hicho cha Januari hadi Juni 2016 ajali zilizosababishwa na ulevi ni 48 sawa na asilimia 41.

Kwa mujibu wa Kamanda Mpinga ofisi yake imechukua hatua kadhaa za kupunguza na hatimaye kumaliza kabisa ajali za barabarani akisisitiza kuwa suala la ajali za barabarani ni jukumu letu na siyo suala la mamlaka za usalama pekee na litapunguza kama kutakuwa na juhudi za makusudi za wadau wote na watumiaji wa barabara.

Tanzania imetia saina Mpango wa dunia wa kusimamia usalama duniani kuanzia mwaka 2015-2019.

Mpango huu unalenga kupambana na ajali katika kiwango cha kitaifa na kimataifa na unatekelezwa na Wizara ya Afya ikishirikiana na Shirika la Afya Duniani (WHO) na pia unawashirikisha wadau mbalimbali kuelimisha umma.

Taasisi ya Mifupa ya Hospitali ya Taifa Muhimbili (MOI) inakumbwa na idadi kubwa ya wagonjwa kuliko uwezo wake. Na hii inatokana na idadi kubwa ya wagonjwa wa ajali ambao wanaishia kwenye chumba cha dharura hospitalini hapo.

Kwa mujibu wa mtaalamu wa kitengo cha ganzi na nusu kaputi wa MOI Daktari Respicious Boniface, kati ya mwezi Januari na Julai 2016, jumla ya wagonjwa 2,520 walioumia kwenye ajali wamehudumiwa, ambao ni sawa na wastani wa wagonjwa 12 kwa siku.

Tatizo linaonekana kuwa linaongezeka ukilinganisha na mwaka uliopita ambapo tulikuwa na wastani wa wagonjwa 9 kwa siku. Sehemu kubwa ya waathirika (Asilimia 70.2) ni watu wa kundi la wazalishaji (Miaka 18 hadi 45) kwa wastani wa mwaname kwa mwanamke ni 3:1. Pikipiki ndizo zilikuwa chanzo cha ajali nyingi za barabarani kwa asilimia 53.4, zikifuatiwa zile za magari ambazo ni asilimia 42.5.

Dk Boniface alimwambia mwandishi wa makala haya kwamba wiki mbili zilizopita hapa Dar es salaam takribani madereva 38.3% ndiyo sehemu kubwa ya wahanga, wakifuatiwa na

abiria 35.4%. Kati ya wagonjwa 2,520 waliohudumiwa, 57.4% walilazwa, 40.4% walitibiwa na wakarudishwa nyumbani na 2.2% walifariki papo hapo ajalini.

Ajali zinazosababishwa na ulevi ziliripotiwa kuwa ni wahanga wapatao asilimia 21.7%, hivyo kuonyesha kuwa unywaji pombe na kuendesha vyombo vya moto ni moja ya sababu kubwa za kutokea kwa ajali za barabarani.

Hali kadhalika, waathirika wengi pamoja na madereva mara kwa mara wanalazwa wakiwa wamelewa sana.

Hata hivyo, hakuna namna ya kupima kiwango cha pombe kilicho katika damu katika hospitali zote na watafiti wa pumzi hawatumi ipasavyo na jeshi la polisi hapa nchini na hii inaweza kuwa ni moja ya vyanzo vya kushindwa kuripoti matukio haya ipasavyo.

Daktari Museru Mcharo wa Chuo Kikuu cha Sayansi ya Tiba cha Muhimbili (MUHAS) ukusanyaji wa takwimu za jeshi la polisi uimarishwe na pia uunganishwe na Takwimu za Afya.

Kwa mujibu wa Dk. Mcharo, takwimu hizo zitatoa taarifa ya aina ya msaada wa lazima unaohitajika katika hatua mbalimbali kabla na baada ya ajali kutokea na zitaonesha taarifa halisi juu ya kiwango cha majeraha yatokanayo na ajali nchini.

Licha ya kuongezeka kwa ajali kulikooneshwa na takwimu zilizopo, majeraha yanayosababishwa na ajali za barabarani bado hayatibiwi ipasavyo kwenye nchi zinazoendelea. Kutokuwepo kwa takwimu sahihi na huduma duni za afya huenda ikawa sehemu ya tatizo.

Sehemu kubwa ya taarifa zinazopatikana kuhusu majeruhi wa barabara za barabarani zimeegemezwa kwenye baadhi ya hospitali zilizochaguliwa hapa Dar es salaam, kwa sababu hii haziwezi kusadifu picha halisi wa tatizo hili hata Dar es Salaam yenyewe. ■

## Sera ya Vileo inahitajika kuthibiti unywaji holela

« pg 17

Bwaba Gama anasema kwamba sera ya pombe ni muhimu katika kuyabana makampuni ya vileo kupunguza unywaji wa pombe kwa sababu ina madhara makubwa kwa vijana ambao ndio nguvu kazi ya taifa

Aliongeza kwamba sera ya udhibiti wa pombe ikifanikiwa nchi itapata fursa kupitia bunge kutunga sheria dhidi ya uuzaji na usambazaji holela wa pombe kwenye jamii ya kitanzania.

Mratibu wa Kituo cha Usuluhishi cha TAMWA Bi Gladness Munuo anayalaumu makampuni ya pombe kwa kutumia ushawishi mkubwa na mikakati ya masoko kufikia wateja wao ambao in wanywa pombe.

“Makampuni yanayozalisha pombe yanafanya hujuma kupinga sera ya taifa ya pombe. Nadhani pamoja na makampuni haya tunahitaji kuweka mkakati wa pamoja ili kupunguza tatizo la ulevi,” Bi Munuo anasema.

Akijibu swali juu ya sera hiyo, Mkuu wa kitengo cha Afya ya akili na madawa ya kulevya Daktari Sabuni anasema sera iko katika mchakato, akibainisha kuwa ipo tayari kwa hatua ya awali, na itawasilishwa kwa wadau kwa majadiliano zaidi.

Wakati serikali inaendelea kuandaa sera hii, wadau wanaonya kwamba hoja hii ni lazima iharakishwe ili ilete ufanisi katika kushughulikia madhara ya kunywa pombe na madhara yake. ■



Kijana akiwa amelewa chakari baada ya kunywa idadi kubwa ya viroba

Na Deus Ngowi

**S**i rahisi kumkuta Almasi nyumbani kwake, na hata ukimkuta ni vigumu kuwa na majadiliano naye kutokana na ukweli kwamba ama hamtaelewana au atakuwa ameishia usingizini.

Almasi (Si jina lake halisi) hutumia muda wake mwingi kwenye baa na mitaa ya kata yake akitafuta jinsi ya kupata aina yoyote ya kilevi kukata kiu yake. Kijana huyu hunywa aina yoyote ya kilevi anachopata, iwe pombe ya kienyeji au hizi za kisasa na hajali iwapo kinywaji husika ni halali kisheria au batili.

Katika mitaa ya kata ya Tuangoma, Tarafa ya Mbagala, Manispaa ya Temeke, Almasi hutafuta Wasamaria wanaoweza kumpatia kinywaji na yupo tayari kukaa na Wasamaria hao kwa muda wowote, ili mradi anajua kwamba hatimaye atapatwa kinywaji.

Ukimwalia Almasi unaweza kudhani kwamba ni mtu mwenye umri mkubwa kutokana na umbo lake la udhoofu, na jinsi afya yake ilivyotererika, rangi ya nywele zake, na anavyotembea.

Nilishangazwa sana shangazi yake Chiku (si jina lake halisi) alivyonimbia kwamba ana umri wa miaka 23 tu, akisema mpwa wake huyo ana hali hiyo kutokana na utumiaji wa kilevi uliopitiliza.

Tangu alipohitimu elimu ya shule ya msingi mwaka 2008 alijiingiza katika shughuli za uchuuzi kabla ya kwenda kufanya kazi katika Soko la Mbagala, akiwa kibega, kwa maana ya kubeba mizigo ya wafanyabiashara kutoka sehemu moja kwenda nyingine, asubuhi na baadaye jioni wakati wa kufunga biashara.

Chiku anasema kwamba kadri muda ulivyokwenda Almasi alianza kutumia kilevi, akiongeza kiasi na kisha akaanza kushindwa kutekeleza majukumu yake inavyotakiwa, akawa anaeleza kazini kwake kwamba anaumwa na akiona ahueni alienda kazini, lakini ikawa ni kwa siku chache za wiki anaweza kwenda kazini.

“Tumeshamzoea katika hali hii sasa lakini baada ya kuhitimu shule alikuwa kijana mchapa kazi mzur, akitafuta fedha kwanza katika biashara na baadaye akifanya kazi kwenye Soko la Mbagala. Kwa sasa yuko hivyo tu lakini jambo la kushangaza ni kwamba hakosi kinywaji chake kila siku; unashindwa kuelewa ni wapi anapata fedha lakini nahisi ni kwa rafiki zake. Kwa sasa pombe imemtawala kabisa na sijui kama ataweza kuondokana na hali hii,” anasema Chiku anayeishi na mpwa wake huyo.

Kaimu Mwenyekiti wa Mtaa wa Goroka, Isa Mtuwa anasema kwamba hali hiyo imemfanya Almasi kutegemea watu wengine wakati ukweli ni kwamba angeweza kuwa ama shuleni au akifanya kazi kwa ajili ya kujipatia kipato bila tatizo lolote.

“Haya ni matokeo ya kutumia kilevi kupita kiasi; hawezi kufanya kazi, afya yake imeathirika kwa sababu hawezi hata kujiamulia vyema kipi cha kufanya. Mbaya zaidi ni kwamba tunapoteza nguvukazi na simwoni kwamba eti siku moja atakuja kuoa, labda apate tiba kutoka kwa wataalamu waliobobea ili aondokane na hali hii,” anasema Mtuwa.

» pg 21



“Sina tatizo lolote lile ili mradi nipate kinywaji changu na nyama choma kidogo. Sina tatizo. Nipo sawa. Nipe kiroba tu kinatosha,” ndivyo anavyomjibu mwandishi wa makala hii.

Dk Kondo Chilonga, Mkuu wa Idara ya Upasuaji katika Hospitali ya Rufaa ya KCMC anaonya dhidi ya matumizi ya kilevi kupita kiasi. Anasema baadhi ya sababu za watu kupenda kutumia kilevi kuwa ni ukosefu wa ajira na pia kutojituma kwao na hivyo huishia kuingia kwenye ulevi.

Anasema kwamba tatizo hilo linaweza kuwa kubwa zaidi kwa vijana kutokana na ukweli kwamba kiwango cha ukosefu wa ajira ni kikubwa kwao na kwamba baadhi yao wanataka kazi za ajira rasmi kukaa ofisini badala ya kujiajiri au kuunda vikundi vya ushirika. Anasema kwamba baadhi yao wana mawazo au kuchanganyikiwa na wanataka wawe kama wengine waliofanikiwa hivyo huishia kwenye ulevi kama njia ya kujipooza.

Dk Chilonga anasema kwamba athari za ulevi kwa wanadamu hutegemea na aina ya kinywaji, vitu vinavyotumika kuvitengeneza, njia za utengenezaji na asilimia ya kilevi chenyewe. Anasema utumiaji uliokithiri huingiza sumu mwilini ambazo hutakiwa kuondolewa. Hiyo inamaanisha kwamba viungo kama ini na figo hufanya kazi ya ziada kwa ajili hiyo na matokeo yake viungo hivyo hufika mahali na kufanya kazi chini ya kiwango au kushindwa kabisa kufanya kazi, ndio ugonjwa wa figo na ini na hufika mahali mhusika akafa.

“Unaweza kutambua viungo hivyo kuanza kushindwa kufanya kazi kwa mhusika kuvimba tumbo, ambapo watu wanaweza kudhani kwamba ana afya nzuri lakini ukweli ni kwamba ni maradhi na sehemu nyingine za mwili zitakuwa dhaifu. Kongosho nalo linaweza kudhurika kutokana na mambo hayo na mlevi huweza kupata kisukari kwani insulin hushindwa kuzalishwa inavyotakiwa,” anasema Dk Chilonga.

Mtaalamu huyo anabainisha pia kwamba kunywa kilevi kabla ya Sauti ya Siti

## Ulevi wakatisha ndoto za vijana



kupata mlo kamili huweza pia kusababisha utapiamlo, vidonda vya tumbo na huenda hali ikawa mbaya na kupelekea saratani.

Dk Chilonga anasema kupungukiwa chembechembe nyekundu za damu zinazotakiwa ni kwa sababu ya kukosa mlo na kwamba ulevi pia husababisha mparaganyiko wa mfumo wa neva unaosababisha mtu kushindwa kufikiri na kuchambua mambo vyema.

“Kufika hatua hii tunaweza kusema kwamba mhusika amekuwa tegemezi na hali hii ni mbaya kwa sababu mtu huyo huwa hutegemea kilevi na hali hiyo huathiri mambo mengi karika jamii,” anabainisha.

Simulizi kuhusu athari za ulevi haziishii hapa; Dk Chilonga anasema kwamba hatua nyingine ni kwamba mfumo wa misuli nao huathiriwa, ambapo mhusika hushindwa kuandika au kushika kitu vyema. Huathiri jinsi mwili wa mhusika unavyojibu kuendana na hali mbalimbali na hudhuru jinsi ya kufanya uamuzi.

Pia, kuna mabadiliko katika kuchukua hatua na anaweza kuonekana kwenye namna ya kuzungumza, kuendesha chombo au kufanya kazi.

Juu ya athari kijamii, unywaji pombe kupita kiasi kwa vijana kunaweza kuwasababisha kushindwa kujenga familia kwa sababu hawatapata nguvu za uzazi kwa hiyo hawatakuwa na watoto kutokana na wingi wa pombe wanayotumia.

Dk Chilonga anasema kwamba kwa wasichana nako kuna athari hasi kwenye unywaji pombe kupita kiasi kwani wajawazito huweza kufikia hatua ya mimba kuharibika na hata wakifanikiwa kujifungua watoto huwa na uzito mdogo sana na akili yao kudumaa.

Kiuchumi, Profesa Honest Ngowi wa Chuo Kikuu Mzumbe anasema kwamba vijana wanaotumia kilevi kupita kiasi hawawezi kushiriki kikamilifu, au hata kidogo, kwenye shughuli za uchumi nchini.

“Hii inakuwa upotevu wa nguvu kazi ambayo vinginevyo ingetumiwa kwa ajili ya uzalishaji wa bidhaa na utoaji huduma kwa ajili ya kukuza uchumi wa nchi na faida zitokanazo kama kodi na mapato mengine yasiyokuwa ya kodi,” anasema.

Akihusisha hilo na nguvu kazi inayopotea, Profesa Ngowi anasema, mapato hupotea kwa sababu wangekuwa wanafanya kazi wangeingiza kipato na kukuza kiwango cha maisha yao kwa kununua bidhaa na huduma zenye kiwango kikubwa. Anasema wasipofanya kazi rasmi huweza kujiingiza kwenye vitu batili kama wizi na ujambazi.

Profesa Ngowi anasema kwamba zipo athari za afya pia, akieleza kwamba unywaji wa pombe nyingi mno hunyong’onyeza afya na kusababisha taifa kutumia kiasi kikubwa cha fedha kwenye matibabu.

“Ikiwa unatakiwa kupatiwa matibabu, inatakiwa pato la taifa kuelekezwa kwenye matibabu badala ya kutumika kwenye shughuli nyingine za maendeleo na huu ni upotevu,” anasema.

Anasema kwamba ulevi miongoni mwa vijana husababisha fujo na vurugu na kuathiri uchumi kuanzia kwa mtu binafsi, kaya na taifa kwa ujumla. ■

# Mikumbo inavyowavuta vijana kwenye ulevi

Na Anastazia Anyimike

**K**ATIKA baadhi ya tamaduni za mataifa mengi ya Afrika, pombe ina umuhimu katika maisha ikiwa ni kwenye sherehe

za ndoa, misiba, na hata wakatiwa utatuzi wa shida mbalimbali katika jamii.

Watu wengi wamekuwa wakijiingiza kwenye unywaji pombe bila kufikiri, jambo ambalo linafanya pombe kuwa ni moja ya vilevi hatari duniani.

Kwa mujibu wa utafiti wa kwanza wa kitaalamu wa mwaka 2015 uliofanywa na Serikali kwa msaada wa Shirika la Afya Duniani (WHO) hatua mbalimbali zinapaswa kuchukuliwa kuepusha vijana na athari za pombe.

►► pg 23



Vijana wakijiburudisha na bia

Utafiti huo ambao uliangalia magonjwa yasiyoambukizwa ambapo matumizi ya pombe ikiwa kama moja ya visababishi, unaonesha kuwa asilimia 29 ya watazania wanatumia pombe kati ya hao wanaume ni asilimia 38.3 na wanawake asilimia 20.9. ambao hawanywi kabisa ni asilimia 51, wanaume ikiwa ni asilimia 43.1 na wanawake asilimia 58.5.

Utafiti huo pia ulionyesha kuwa wanywaji pombe wa kila siku ni asilimia 11, wanaume asilimia 13.6 na wanawake asilimia 8.2. utafiti ulionyesha ongezeko la unywaji pombe wa kila siku hasa kwa watu wenye umri kati ya miaka 55-64 kuwa ni asilimia 25 huku vijana wa umri wa kati ya miaka 25 hadi 34 ni asilimia saba.

Daktari Fredrick Mashila ambaye ni mtaalamu wa Fisiolojia ya homoni na mazoezi katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili anasema watu wanatakiwa kuwa makini na wasiige unywaji wa pombe kwa mtu mwingine kutokana na kuwa kila mwili wa mtu una namna yake ya kuhimili pombe anayokunywa.

“Kuna miili ambayo ina uvumilivu mdogo, na ndio maana mtu anaweza kunywa bia moja na akaharibikiwa kabisa, na mwingine akanywa nyingi akawa mzima.

Anaongeza kusema kuwa watu ambao miili yao haiwezi kuhimili pombe, wanakuwa na hatari kubwa ya kupata madhara kwa sababu miili yao inavinasaba ambavyo vinashindwa kuvunja vunja pombe hivyo kuenea zaidi mwilini. Hivyo usiige unywaji wa mtu ukadhani watu wote wako sawa, watu tunatofautiana na miili kuvumilia pombe pia inatofautiana”.

Daktari Mashila anasema takwimu zinaonesha kuwa idadi kubwa ya watu kuanzia miaka 15 na kuendelea ndio wanywaji wa pombe wa wastani wa lita 6.3 hadi lita 6.7 kwa mtu kila siku.

“Pombe inachangia sana vifo na magonjwa kama ya ini, saratani, kisukari, magonjwa ya akili na unene uliokithiri. Takwimu za Shirika la Afya

# Mikumbo inavyowavuta vijana kwenye ulevi



Duniani zinaonesha kuwa asilimia tano ya vifo yote duniani vinatokana na pombe ambayo ni zaidi ya milioni 3.3.” anasema.

Daktari Mashila anaongeza kusema kuwa jambo ambalo watu hawataki kulizungumzia ni ukweli pia kwamba ukinywa pombe kiasi ambacho kinakubalika kiasya ina faida kwa mtumiaji kuliko wale wasiokunywa.

“Wataalamu wakiwemo madaktari wanashindwa kuzungumzia manufaa ya pombe kwa sababu watu wengi wanapokunywa hawazingatii kiwango kinachotakiwa kiasya. Hata hivyo, uzoefu na tafiti zilizofanyika zinaonesha kuna kiwango ambacho mnywaji pombe akitumia kinamfanya mtu kuwa na afya njema” anasema na kubainisha kuwa pombe aina ya mvinyo hususani ile nyekundu isiyo na nyongeza ya sukari ina manufaa zaidi kwenye mwili wa binadamu.

Kwa ujumla ni vizuri kuepuka matumizi ya pombe. Lakini iwapo imebidi unywaji pombe, basi kwa siku isizidi kipimo kimoja kwa mwanamke na kwa wanaume isizidi vipimo viwili.

Makadirio ya kipimo kimoja ni bia ya kawaida, ambayo ni glasi moja ya wastani wa milimita 250, mvinyo glasi moja ndogo ambayo ni ml 100, vinywaji vikali kama konyagi, whisky au brand ni mililita 25. Kwa mfano, bia nyingi hapa nchini zina ujazo

wa mililita 500, hivyo mwanamke anatakiwa kunywa nusu ya ujazo huo na mwanamume bia moja kwa siku.

“Kiwango cha pombe inayokubalika kiasya inatofautiana na aina ya kilevi kilichomondaniya pombe hiyo. Mfano mvinyo kiwango kinachokubalika ni glasi moja kwa mwanamke na glasi mbili kwa mwanamume. Glasi haitakiwi iwe imejaa, ukizidisha hapo tayari unaingia kwenye matatizo ya kiasya.

Anasema, pombe za kienyeji kutokuwa na viwango na kuandaliwa katika mazingira yasiyoridhisha zinachangia magonjwa ya kuambukiza. Magonjwa kama Kifua Kikuu (TB) na Ukimwi hutokana na wanywaji kukosa umakini na kushindwa kufanya maamuzi sahihi.

Mtu hatakiwi kunywa pombe pale anapotumia dawa zinazokinzana na pombe. Mfano dawa za flagil, antibiotics. Hivyo chukua tahadhari kwa unywaji wa pombe.

Dk Mashila anasema dhana ya kuwa pombe kali hutibu mafua au kuondoa mafuta mwilini ni potofu. Watu wanatakiwa waache dhana hizo kinyume chake wanaweza kupata madhara makubwa kwenye mwili.

Anapozungumzia suala la mafua, anasema mafua yanatokana na virusi ambavyo kwa kawaida havina tiba. ■



Wakati mwingine, ugomvi ndani ya familia husababishwa na pombe

# Pombe inasababisha migogoro ndani ya familia

Na Editha Majura

**K**ATIKA benchi lililo mkabala na mlango wa kuingilia kwenye ofisi ya ustawi wa jamii, wilayani Kinondoni wameketi wanawake watatu wakisubiri wanaohudumiwa watoke ofisini nao waingie.

Alisia Melikioli (siyo jina halisi), mwenye umri wa Miaka 40 na watoto watatu; Mmoja wa kiume, Wawili wa wakike anasikika akieleza wenzakekuhusu kilichompeleka kwenye ofisi hizo.

Anasema anahitaji kupewa barua itakayowahakikishia usalama wasamaria wema, ambao wamemuhifadhi kwa siku kadhaa tangu alipohama nyumbani kwake, kuepuka kipigo alichokuwa akishushiwa na mume wake.

Anasimulia kwamba tangu aolewe na mwanaume huyo kwa ndoa ya Kikatoliki, amekuwa mtu wa kupigwa hata mbele za watoto wake na sasa ameshindwa kuendelea kuvumilia.

Anatoa rundo la vyeti vya hospitalini na kuwaonesha wenzake akisema, "Vyote hivi ni vyeti vya hospitali mbalimbali nilikotibiwa kutokana na vipigo ninavyovipata kutoka kwa mwanaume huyu wakati amelewa" anasema.

Anasimulia anavyoumizwa na hatua ya kuacha makazi na watoto wake kwa mwanaume huyo, ambaye sasa ameanza kutishia usalama wa wasamaria wema waliomuhifadhi mkewe.

Inaashiria amechelewa kufanya uamuzi huo, kwani anabainisha kuwa tayari mguu wake wa upande wa kushoto, ulivunjwa katika moja ya matukio ya kupigwa na mume wake huyo.

Pia inaashiria ameathirika kisaikolojia, hawezi kuzungumza kwa mtiririko mzuri bila kuvuta kumbukumbu.

Ingawa anasikitishwa kuishi mithiri ya mkimbizi nchini mwake, anasema kinachoumiza zaidi ni kumtengana na watoto wake, kutokana na ukatili wa baba yao.

Kisa cha Alisia ni kimoja miongoni mwa vingi ambavyo hufikishwa katika idara ya Ustawi Wa Jamii hapo Kinondoni.

Afisa Ustawi wa Jamii katika Manispaa ya Kinondoni, Judith Kimaro, anasema unywaji pombe unaathiri sana mahusiano katika familia na wakati mwingine huzisambaratisha

Anasema ndoa nyingi zimeingia katika migogoro na baadhi kuvunja kufuatia wanawake kujihusisha na ukahaba pindi waume zao wanapokuwa safarini kikazi.

» pg 25





“Januari hadi Oktoba mwaka jana tulipokea ndoa 12 wanawake wakituhumiwa kufanya ulevi na ukahaba hasa nyakati za jioni, pindi waume zao wanaposafiri kikazi na wengi wao wakiwa wameambukizwa magonjwa ya zinaa na ukimwi” anaeleza Kimaro.

Anasema kuwa hasara zitokanazo na ulevi wa pombe ni pamoja na wazazi wote au mmoja kutelekeza familia, hata asipohama nyumbani lakini kushindwa kutimiza majukumu ya wazazi.

Anatoa mfano wa kesi zilizopokewa na ofisi hiyo kati ya Januari na Desemba mwaka jana, kuwa ni 720 ambapo kati ya hizo 213 kiini chake ni ulevi wanandoa kunywa pombe na kuasabisha migogoro ndani ya ndoa zao.

Kati ya kesi 150 zilizosuluhishwa na ofisi hiyo ni 63 huku zilizosalia zikipelekwa katika mamlaka nyingine, kama vile Baraza la usuruhishi la ndoa na mahakamani.

Kimaro anasema Watoto na Mama wanapokosa, ikiwa Baba amekunywa pombe wanapata kipigo kupita kiasi tofauti na ambavyo angekuwa katika hali ya kawaida.

Anatoa mfano wa mtoto aliyejeruhiwa mwilini baada ya baba yake mzazi, kumpiga kwa kutumia waya wa umeme kwasababu mtoto hakufanya ‘Home Work’ aliyopewa na walimu shuleni.

Anasema wanawake na watoto wamekuwa waathirika wakubwa wa udharilishaji wa kingono unaofanywa na wanaume, ambapo baadhi huwa katika hali ya ulevi.

Anatoa mfano wa mwanaume ambaye kila aliporejea nyumbani akiwa amelewa, alitaka kufanya mapenzi na mtoto wa kike mwenye umri wa miaka saba.

“Baba huyu alikuwa na tabia ya kumning’iniza mtoto kichwa chini miguu juu na baada ya dakika kadhaa anamlazimisha kujamiiana naye kwa

# Pombe inasababisha migogoro ndani ya familia



nguvu,” anabainisha afisa huyo wa ustawi wa jamii.

Tangu Juni mpaka Oktoba mwaka jana, anasema walipokelewa kesi tano za udharilishaji wa aina hiyo kwa watoto na kwamba Mbili kati ya hizo, zilizuluhishwa na Tatu zilipelekwa mahakamani.

Anasema ofisi hiyo pia inazo kesi zinazohusisha Baba au Mama wa familia, kwenda sehemu za kuuzia pombe (Bar) na kurejea nyumbani usiku wa manane, akiwa amelewa chakari.

“Mfano tangu Agosti mpaka Septemba mwaka jana, tulipokea kesi za aina hiyo Tano, familia zenye wazazi wa aina hii zinakosa furaha na amani,” anaeleza.

Anasema ongezeko la watoto wasiokuwa na Baba au Mama au

wazazi wote wawili, ni kubwa katika jamii ya Tanzania.

Unywaji pombe wa kupindukia, unaelezwa kuwa moja ya sababu kubwa ya tatizo hilo.

Anatoa mfano wa watoto Watano walioachwa yatima, baada ya Baba yao kuugua magonjwa ya figo na Ini, huku Mama yao naye akiugua moyo kutokana na kunywa pombe kali kwa muda mrefu huku wakiwa hawali chakula.

Anasema kati ya Kata 10 za Manispaa ya Kinondoni, kuna watoto yatima 6,533 ambao wametambuliwa rasmi mbali na wale ambao hawatambuliwa.

Anasema yatima 2,000 wamepoteza wazazi kwa ajali, magonjwa mbalimbali ikiwemo HIV/AIDS ambapo imebainika kuwa kwa namna tofauti, ulevi ni chanzo cha janga hilo.

Maeneo yanayoongoza kwa kuwa na watoto wa mitaani wengi katika Manispaa ya Kinondoni, yanatajwa na Kimaro kuwa ni Daraja la Salenda, Jangwani, Morocco na maeneo karibu na kanisa la Mtakatifu Petro Oysterbay.

Anasema tangu Januari mpaka Oktoba mwaka jana, walisikiliza kesi za watoto hao 220 ambao walifika maeneo mbalimbali ya manispaa hiyo wakitokea Dodoma, Singida na Wilaya ya Pangani mkoani Tanga.

Pamoja na sababu nyingine, wazazi kuendelea ulevi na kushindwa kutimiza majuku yao ya msingi kwa familia, inatajwa kuwa sababu ya ongezeko la watoto wa mitaani nchini.

Kutokana na madhara yanayotokana na unywaji pombe, ofisi ya ustawi wa jamii Kinondoni inashauri elimu kuhusu madhara ya unywaji pombe itolewe kwa jamii nzima.

Elimu itolewe kwa mtu mmoja mmoja, familia na makundi mbalimbali ya watu ili waweze kufahamu kwa hakika, uhalisia wa hatari inayolikabili taifa kutokana na unywaji wa pombe.



# Uuzaji holela wa vileo walalamikiwa

NA RUTH MNKENI, DAR ES SALAAM

BAADHI ya wakazi wa Jiji la Dar es Salaam wamelalamikiwa baadhi wauzaji wa vileo kutokuzingatia sheria za biashara hiyo.

Wakizunguma na MTANZANIA kwa nyakati tofauti, walisema baadhi ya baa zimeendelea kufunguliwa bila utaratibu, jambo ambalo ni changamoto katika jamii.

Mmoja wa wakazi hao ambaye ni mkazi wa Wilaya ya Kinondoni, Hawa Komba, alisema ni baa nyingi zimekuwa

zifikunguliwa mapema na kuchelewa kufungwa, tofauti na sheria ya uuzaji wa vileo ya mwaka 2009 inavyooleza.

"Mfano ni baa zilizopo karibu na vituo vya polisi zinavunja sheria hivo huku jeshi hilo likiangalia bila kuchukua hatua yoyote. Inabidi suala hili tufikeme kwa nguvu zote ili kuiepusha jamii na familia zetu kujiingiza katika uelevi uliokithiri," alisema Hawa.

Aliongeza kuwa wafanyabiashara wa vileo hawako makini katika kufuata sheria ya kazi zao na hivyo ni vema vyombo vya dola vichukue

hatua stahiki ya kuhakikisha sheria zinazingatwa.

Naye mwanaharakati, Mohamedi Chunga, alisema ni wakati muafaka sheria ichukue mkondo wake, kwani unywaji wa pombe kupita kiasi unachangia kudimiza uchumi wa mtu mmojammoja na taifa kwa ujumla.

Kwa upande wake, Kamishna wa Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, Simoni Sirro, akizunguma na MTANZANIA kwa njia ya simu, aliwatahadharisha wafanyabiashara wa vileo kufuata sheria ya muda

uliopangwa.

Alisema yeyote atakayekiuka maagizo hayo hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake, ikiwa ni pamoja na kufunguliwa biashara yake.

"Upo mtindo wa wahudumu wa baa kufungulia muziki mkubwa, hali inayosababisha wananchi waliopo karibu na eneo hilo kukosa usingizi kutokana na sauti kubwa," alisema Sirro.

Alisisitiza kuwa ni marufuku kufungulia muziki mkubwa ambao unawaumiza watu na kushindwa kuendelea na shughuli zao.

MTANZANIA MARCH 28, 2016 Pg 24



Habari/Tangazo  
Majira 24/3/2016 pg 8

## 'Ukatili unaotokana na unywaji pombe kupindukia ufichuliwe'

Na Mwandishi Weta

■ ■ ■ **WYOMBO** vya habari nchini vimetakiwa kuwa mistari wa mbele kuripoti matukio ya ukatili wa kijinsia unaoSababishwa na unywaji pombe kupindukia ili kuhakikisha watu wote wanapitia kwenye unywasaji huo wanagaliwa na kupiwa msada katika mamlaka husika.

Ushauri huo ulitolewa Dar es Salaam juzi na Ofisi Habari wa Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA), Happiness Bagambi, wakati akitoa mada kwenye mkutano wa ekumu moja kuhusu mchango wa vyombo vya habari na jamii, uhusiano na ukatili wa kijinsia unaoSababishwa na unywaji pombe na madhara yake kwa ujumla.

Lengo la mkutano huo uliowakutanisha waandishi wa habari na wadau wengine ilikuwa ni jinsi ya kutoa huduma kwa waathirika wa ukatili wa kijinsia unaoSababishwa na unywaji pombe kupita kiasi, ambapo mradi huo unatekelewa katika kazi tatu za Sirarigi, Makumbusho na Wazo, zote za Kinondoni, Dar es

Salaam kwa kuratibiwa na TAMWA na kwa kufadhiliwa na IOGT.

Bagambi, alisema bila vyombo vya habari, si rahisi kufahamu machara yanayosababishwa na unywaji pombe kupita kiasi.

Unywaji pombe kupita kiasi ni tatizo, kwani wanawake wamekuwa wakifanyiwa viendo vya unywasaji, lakini wanaona aibu kama ukatili wanaofanyiwa," alisema Bagambi.

Alisema, waandishi wa habari wanatakiwa kuelewa kwa kina dhana nzima ya unywasaji wa kijinsia unaoTokana na pombe ili waweze kuiba mikakati inayoweza kuwasaidia waathirika kupata ulina.

Kwa mujibu wa Bagambi, **W A N A K E W E N G I** wanaopigwa na wanume kutokana na suruya pombe kurudi kiasi wanapokuwa na nguvu kutokana na yipigo, lakini hawasemi ukweli badala yake wanadai wameleleza na kuong'aa.

Ni kuong'aa kwa namna gani huko hadi licho linatoka? alihoji Bagambi na kuong'aa kwamba madawati ya jinsia katika Jeshi la Polisi yanawasaidia kueleza chanzo cha kesi hizo.

Kwa mantiki, hiyo alisema waandishi wa habari ni koo cha jamii, hivyo angopewa kufahamu kwamba vyombo vya habari vinatana kazi kwa ajili ya jamii, taifa na ulimwengu mzima.

Aliwataka waandishi wa habari nchini kuhakikisha wanaandika kwa lina ukatili wa kijinsia unaoTokana na unywaji pombe kwani wao ndiyo sauti ya watu waostokika.

"Kwa maingi huo vyombo vya habari vina nafasi ya kufichua maovu katika jamii na kusaidia kuyepatia ufumbuzi," alisema.

Wakati huo huo, Bagambi, aliwataka Wataendaji wa Serikali za Mitaa kuhakikisha wanashughulika ipasavyo ukatili wa kijinsia unaoTokana na unywaji pombe kupindukia.

"Huko mnakoishi ndiko kuna matukio mengi ya ukatili yanayotokana na unywaji pombe kupindukia, kwa hivyo wakisia waandishi wa habari, wape ushikano, kwani ukatili wa aina hii unauimiza familia," alisema Bagambi na kusisitiza.

Tushirikiane kuondoa ukatili wa aina hii ili tuwe na Tanzania yenye amani inayoheshimu haki za binadamu."